# Nipashe

Jumanne Julai 28, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580295

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wastaafu, wakuu wa taasisi waeleza kumbukumbu alizoacha

UKURASA 3




UKURASA 11

# DAR KUSIMAMA

UKURASA 2



Waziri Mkuu wa Burundi, Jenerali Alain Guillaume Bunyoni (kulia), akipokewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, kuhudhuria mazishi ya kitaifa ya Rais mstaafu, Benjamin Mkapa. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Viongozi kimataifa waanza kumiminika

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store



MICHEZO **FIFA KUMSHUKIA EYMAEL** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akilakiwa na wanachama na mashabiki wa chama hicho, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, jana. **Habari Uk. 4.** PICHA: MIRAJI MSALA

# Viongozi kutoka nje waanza kuwasili

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI kutoka nchi mbalimbali wameanza kuwasili nchini kwa ajili ya kushiriki mazishi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamini Mkapa, yatakayofanyika kijijini kwake Lupaso, wilayani Masasi, mkoani Mtwara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Emmanuel Buhohela, kiongozi wa kwanza kuwasili ni Waziri Mkuu wa Burundi, Jenerali Alain Bunyoni.

Kiongozi huyo aliambatana na Spika wa Baraza la Seneti la Burundi na kuwasili majira ya saa 5:20 asubuhi kwa ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania, na kuwa viongozi wa kwanza kutoka mataifa ya nje kuwasili nchini.

"Burundi imepokea kwa mshtuko na majonzi makubwa taarifa za kifo cha Mkapa, kutokana na urafiki wa kindugu baina ya Tanzania na Burundi, amekuja nchini kuwawakilisha Warundi kuomboleza na Watanzania, alisema."

Spika Reverien Ndikuriyo alisema kifo kimeyapokonya maisha ya hayati Mkapa ambayo bado alikuwa akihitajika kwa kiasi kikubwa hususani katika Bara la Afrika kutokana na uwezo wake mkubwa katika usuluhishi na hivyo Burundi imempoteza msuluhishi mkubwa.

Pia, kiongozi huyo aliambatana na Naibu Mkuu wa Chama Tawala nchini Burundi cha CNDDFDD, Joseph Ntakarutimana.

Akizungumza baada ya kuwapokea viongozi hao, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema wageni hao wamewasili mkoani Kigoma na baadaye kupanda ndege ya ATCL kuja Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Kabudi, ujio wa viongozi hao unaidhihirishia dunia uhusiano mwema na wa kindugu uliopo kati ya Tanzania na Burundi bila kujali nyakati za shida, maombolezo ama raha.

# D'Salaam kusimama mazishi ya Mkapa

**Na Joseph Mwendapole**

SHUGHULI katika Jiji la Dar es Salaam zinatarajiwa kusimama kwa muda leo kupisha mazishi ya kitaifa ya Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, aliyefariki dunia kwa mshtuko wa moyo usiku wa kuamkia Ijumaa.

Mazishi ya kitaifa ya kiongozi huyo yanatarajiwa kufanyika kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, huku maelfu ya Watanzania na wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani wakitarajiwa kuhudhuria.

Kutokana na idadi kubwa ya viongozi watakaohudhuria mazishi hayo, barabara nyingi za jiji hilo la kibiashara zinatarajiwa kufungwa kupisha misafara ya viongozi wa kitaifa.

Mbali na misafara ya viongozi wa kitaifa, kunatarajiwa kuwa na misafara ya mabalozi na viongozi wa mataifa na mashirika mbalimbali makubwa duniani ambao wamethibitisha kushiriki kwenye mazishi hayo.

Viongozi wa kitaifa wanaotarajiwa kuwapo kwenye mazishi hayo wakiongozwa na Rais John Magufuli ni pamoja na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Wengine wanaotarajiwa kuhudhuria mazishi hayo ya Mkapa ambaye aliiongoza Tanzania kuanzia mwaka 1995 hadi 2005, ni marais wastaafu, Jakaya Kikwete na Ali Hassan Mwinyi na mawaziri wakuu wastaafu, Edward Lowassa, Frederick Sumaye, Jaji Joseph Warioba, Cleopa Msuya na John Malecela.

Mbali na viongozi hao wa kitaifa, maelfu ya Watanzania watakuwa wakienda kwenye Uwanja wa Uhuru kushuhudia shughuli ya mazishi ya kiongozi huyo, hali ambayo inatarajiwa kusababisha msongamano wa magari, hususan kwenye barabara zinazokwenda uwanjani huko.

Vilevile, Uwanja wa Uhuru wenye uwezo wa kuchukua watu 30,000 unatarajiwa kufurika idadi kubwa ya Watanzania kutoka Jiji la Dar es Salaam na mikoa mbalimbali ambao watajitokeza kwenda kumuaga Mkapa ambaye enzi za utawala wake, alikuwa maarufu kama Mzee wa Uwazi na Ukweli.

**MAGARI MAALUM**

Msemaji wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, aliwaambia waandishi wa habari jijini jana kuwa, wananchi wataanza kuingia kwenye uwanja huo kuanzia saa 12.30 asubuhi na aliwahimiza wawahi ili wapate nafasi.

Dk. Abbas alisema kutokana na idadi kubwa ya watu wanaotarajiwa kujitokeza kwenye shughuli hiyo, serikali imeandaa utaratibu maalum kwa viongozi kwenda kwenye uwanja huo kwa kutumia usafiri wa pamoja wa mabasi kutoka viwanja vya Karimjee hadi Uwanja wa Uhuru.

Alisema viongozi kama mawaziri, manaibu wao, makatibu wakuu na manaibu wao, wakurugenzi wa mashirika ya umma, wakuu wa mikoa na wilaya, viongozi wa vyama vya siasa na wabunge, wanatakiwa kufika mapema na kuyaacha magari yao katika Viwanja vya Karimjee jijini.

"Tunawaomba viongozi hawa wawahi Karimjee waegeshe magari yao pale na wapande usafiri wa pamoja kuelekea Uwanja wa Uhuru na gari la mwisho la pamoja kutoka Karimjee linatarajiwa kuondoa saa 1:30 asubuhi, hivyo tunawaomba wawahi kufika," alisema.

**KUAGWA KAMA NYERERE**

Mazishi ya kitaifa ya kiongozi huyo yanatarajiwa kufanywa kwa staili kama aliyofanyiwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1999. Nyerere aliagiwa katika uwanja huo wakati huo ukiitwa Uwanja wa Taifa. Wakati wa mazishi ya Nyerere, viongozi wa ndani na nje pia walisafirishwa kwa magari maalum kwenda uwanjani.

Sambamba na kufanyikia katika eneo hilo, shughuli ya leo itaanza kwa misa ya wafu itakayofanyika katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Immaculate, Upanga kisha mwili kupelekwa Uwanja wa Uhuru. Misa ya Nyerere ilifanyika katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Joseph na baadaye mwili wake kupelekwa uwanjani kwa mazishi ya kitaifa. Licha ya matukio hayo kufanana, pia katika mazishi hayo ya kitaifa kutakuwa na salamu mbalimbali kutoka kwa viongozi wa ndani na nje ya nchi kama ilivyokuwa kwa Nyerere.

Jambo la tatu linalofanana katika matukio hayo mawili ni mwili kusafirishwa kutoka Uwanja wa Uhuru hadi Uwanja wa Ngege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) tayari kupelekwa Lupaso. Mwili wa Nyerere pia ulitolewa Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru) kwenda JNIA na hatimaye kusafirishwa kwenda Butiama kwa maziko.

**RATIBA YA KUAGA**

Dk. Abbas alisema shughuli ya kumuaga Mkapa inatarajiwa kuanza wakati wowote leo mara tu mwili wake utakapowasili ukitokea kwenye ibada itakayofanyika katika Kanisa la St. Immaculate.

Alisema kuwa katika shughuli hiyo, kutakuwa na hotuba na salamu za rambirambi kutoka kwa mabalozi na wawakilishi wa mashirika mbalimbali duniani ambazo zitasomwa na baada ya hapo mwili utasafirishwa kwenda kijijini kwake Lupaso mkoani Mtwara kwa ajili ya maziko.

"Maziko yatafanyika Jumatano kijijini kwake Lupaso, Wilaya ya Masasi, Mtwara ambapo ibada ya mazishi inatarajiwa kuanza saa 2:30 asubuhi siku hiyo na baadaye maziko kufanyika saa 4:00 asubuhi baada ya taratibu zingine kukamilika," alisema.

HABARI KITAIFA

# Wasimulia alivyoacha alama za kudumu

**Elizabeth Zaya na Enock Charles**

VIONGOZI mbalimbali waliofanya kazi na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, na walioko madarakani sasa, wameelezea mambo kadhaa ambayo kiongozi huyo aliyafanya na yatabaki kumbukumbu ya kudumu.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kupambana na umaskini kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kuanzisha mfumo rasmi wa ukusanyaji kodi chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mkapa ambaye aliongoza nchi kuanzia mwaka 1995 hadi 2005, alifariki usiku wa kuamkia Ijumaa iliyopita jijini Dar es Salaam na atazikwa kesho kijijini kwao, Lupaso, Masasi mkoani Mtwara.

Akizungumza wakati wa kuaga mwili wa Mkapa jana, aliyekuwa Waziri wa Fedha mwaka 2000 hadi 2005, Basil Mramba, alisema kipindi hicho walipanga mipango ya kuwasaidia wananchi kuondokana na umaskini ikiwamo kuanzishwa kwa TASAF.

"Nitamkumbuka kwa mengi na kubwa kuliko yote ni kupambana na umasikini na wakati ule tulikuwa na mipango ya kuondoa umasikini. Siku moja aliniuliza kwamba wewe una uhakika kweli kwamba kila Mtanzania anataka kuondokana na umaskini?" alisema Mramba.

Alisema Mkapa alitaka mtu asaidiwe hatua kwa hatua hadi pale atakapoondokana na umaskini na kwamba aliuchukia umasikini kwa dhati.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mgwhira, alisema kuwa Mkapa alianzisha mfumo wa ukusanyaji kodi chini ya TRA jambo ambalo limesaidia ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi.

Kwa pande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alisema miongoni mwa viongozi ambao anajifunza kutoka kwao ni pamoja na Mkapa.

"Sisi kwenye nafasi hizi za uongozi mara zote huwa kuna waliotutangulia ambao tunapenda kuiga mfano wao na Mzee Mkapa ni mfano wa kuigwa na napenda kuiga japokuwa sijui kama nitamfikia," alisema Malima.

"Lakini kwa mara zote nilizokuwa nakaa naye na hata kwa kumsikiliza, alikuwa na uthubutu na upeo mkubwa wa kufanya maamuzi (uamuzi) na alifanya mambo ambayo amejitosheleza kwa kuyafahamu. sasa viongozi tunaochipukia sasa hivi tuna haja ya kujifunza kutoka kwake."

ALIKUWA DAWA KWA TAIFA

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema uwapo wa viongozi wastaafu ni dawa tosha kwa taifa.

"Mkapa na viongozi wengine wakuu wastaafu wamefanya mengi na makubwa katika taifa hili kwa hiyo uwapo wao hata kama hawasemi chochote, kivuli chao tu kinakuwa kama kinazungumza na wewe na kinakusaidia wewe kiongozi unayekuwa madarakani kujifunza kwao. Kama nilivyosema ni dawa tosha wa taifa na tunakuwa tunajisikia furaha kwa sababu wanategemewa kwa mambo mengi," alisema Simbachawene.

"Tulipata faida kutoka kwa Mkapa kama nchi kwa kuiheshimisha duniani kupitia usuluhishi wa migogoro katika mataifa mbalimbali. Bado mchango wake ulikuwa unahitajika," aliongeza.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema Mkapa ndiye mwasisi wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) ambayo kwa sasa imefanikiwa kupambana na ugonjwa huo kwa kiwango kikubwa.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimetajwa kufanikiwa kupambana na kudhibiti kwa kiwango kikubwa ugonjwa wa Ukimwi, hii ni taasisi ambayo iliasisiwa na Mkapa na kuweka misingi imara ya kupamba na janga hili na sasa ugonjwa huu kwetu siyo tishio tena,"alisema Mhagama.

**KIKULA ATOA NENO**

Naye Makamu Mkuu wa Kwanza wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Profesa Idris Kikula, alisema Mkapa atakumbukwa kwa mambo mengi katika elimu ya juu hasa kuanzishwa kwa chuo hicho.

Alisema uwapo wa chuo hicho ni alama tosha kwamba Mkapa alifanya makubwa katika elimu ya juu hasa kwa uthubutu wake wa kutoa ukumbi wa CCM Chimwaga kwa ajili ya kufanikisha azma hiyo.

**ALIPENDA VYOMBO VYA ULINZI**

Akizungumza msibani hapo aliyekuwa Mkuu wa Majeshi nchini, Davis Mwamunyange, alisema Mkapa alikuwa mtu shupavu na alivipenda vyombo vya ulinzi na uslama. Mwamunyange alisema Mkapa alikuwa karibu sana na vyombo vya ulinzi na usalama na alipendelea kutoa maelekezo ya mara kwa mara namna ya kutekeleza majukumu yake vizuri.





Mapokezi ya Tundu Lissu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tundu Lissu arejea, maelfu wampokea

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amerejea nchini na kupokewa na maelfu ya wanachama na wafuasi wake walioongozwa na viongozi waandamizi.

Lissu (52), alitua kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam jana majira ya saba mchana, akitokea Brussels, Ubelgiji alikokuwa amekwenda kwa ajili ya matibabu ya kibingwa tangu Januari 2018 baada ya shambulio la kupigwa risasi mkoani Dodoma.

Septemba 7, 2017, mtaalamu huyo wa sheria alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana alipokuwa anajiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake jijini Dodoma muda mfupi baada ya kumalizika kwa kikao cha mchana cha Bunge, ambacho alishiriki kuchangia hoja akiwa Mbunge wa Singida Mashariki.

Baada ya kuwasili uwanjani hapo jana, wakati akikamilisha taratibu za safari, wafuasi wa CHADEMA walikuwa wamejipanga ndani na nje ya jengo la Terminal 3 eneo la kutokea wageni wakimngojea huku wakiimba 'Rais...Rais...'

Kulikuwa na kusukumana na kukanyagana pale Lissu alipotoka huku umati huo mkubwa wa watu ukimshangilia, baadhi ya wafuasi wakibeba mabango yenye ujumbe wa kumkaribisha nyumbani.

Lissu, aliyekuwa akitembea kwa kuchechea, alipokewa na viongozi wakuu wa CHADEMA wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, aliyekuwa akitembea kwa msaada wa magongo.

Baada ya kuingia kwenye gari la wazi alilokuwa ameandaliwa, Lissu alisimama kuwasalimia wananchi huku akionyesha vidole viwili juu, akiwabusu na kunyosha mikono juu na kuinama ikiwa ni ishara ya kushukuru.

Msafara wa kutoka uwanjani huko kwenda Makao Makuu ya CHADEMA Kinondoni jijini ulianza saa 2:20 mchana, magari kadhaa yakiongoza huku maelfu ya wafuasi wakitembea na wengine kukimbiza gari la Lissu wakiendelea kuimba nyimbo mbalimbali.

Akiwa kwenye gari hilo la wazi, Lissu alionekana maeneo mbalimbali akiwapungia mikono wananchi na idadi ya wafuasi ilionekana kuongezeka zaidi kuanzia Daraja la Mfugale kuelekea Buguruni ambako msafara huo ulipita huku msafara wake ukisababisha foleni ya magari kwenye maeneo aliyopita jijini.

Magari ya askari wenye silaha za moto yalionekana maeneo yote msafara huo ulikopita kuhakikisha usalama unakuwapo wakati wote.

***Imeandaliwa Romana Mallya, Mary Mshami, Magdalena Haule na Fatma Mtutuma***

# CUF wajifungia kupitisha mgombea wa urais 2020

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), jana kilifanya mkutano wake mkuu ambao pamoja na mambo mengine, ulikuwa na ajenda ya kumpitisha mgombea wa chama hicho kwa nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Zanzibar.

Mkutano huo mkuu ulifanyika jijini Dar es Salaam ukiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Profesa Ibrahim Lipumba.

Akizungumza wakati wa kufungua mkutano huo, Profesa Lipumba alisema ilani ya uchaguzi ya chama hicho bado inaamini katika kutoa kipaumbele cha nchi kuwa na Katiba mpya inayompa Mtanzania uhuru wa kweli wa kuchagua na kuchaguliwa. Alisema chama chao pia kinatilia mkazo umoja wa kitaifa ambao hautakuwa na ubaguzi kwa mtu, akisisitiza kuwa serikali itakayoundwa na chama hicho, itahakikisha inatokomeza njaa na kuimarisha lishe kwa watoto.

Profesa Lipumba alisema chama hicho kitasimamia uchumi na kuhakikisha unakua kwa asilimia 10 kila mwaka ndani ya miaka 10 hadi 15 mfululizo kwa kuweka misingi imara ya kukuza sekta ya kilimo na kuboresha sekta ya viwanda.

Alisema rais wa serikali itakayokuwa inaongozwa na chama hicho, ni lazima ahakikishe anajiwekea malengo katika kipindi chake chote atakachokuwa madarakani, ili baada ya kuondoka, aliletee taifa tuzo ya Mo Ibrahimu kwa mazuri ambayo atakuwa ameyafanya katika nchi.

Akizungumzia kampeni zinazotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu, Profesa Lipumba alisema chama hicho kimejipanga kuhakikisha kinaendesha kampeni za kistaarabu za kujenga hoja.

Profesa Lipumba pia alisema chama hicho hakiingia katika uchaguzi huo kushiriki bali kushinda.

Profesa Lipumba pia alitumia fursa hiyo kuipongeza serikali kwa kutokuifunga nchi kutokana na janga la ugonjwa wa corona, akifafanua:

"Tunaipongeza serikali kwa kutokuifunga nchi kutokana na janga hili. Huu ni uamuzi mzuri kwa sababu tunaona pia watu wanapotea kila siku kutokana na ajali za barabarani na huwezi kusema ufunge watu wasisafiri kwa sababu kuna ajali, isipokuwa unapaswa kutafuta njia ya kuzuia hilo lisitokee."

**KUKOSA FURAHA**

Profesa Lipumba pia alizungumzia suala la wananchi kukosa fursa, akinukuu utafiti uliobainisha kuwa nchi inashika nafasi ya 148 kati ya nchi 153 ambazo watu wake hawana furaha duniani.

Alisema wananchi kukosa furaha kunachagizwa na hali ngumu ya maisha, akibainisha kuwa asilimia 74 ya watoto wa kitanzania wanaishi katika umaskini.

Profesa Lipumba alisema wachambuzi wengi wa maendeleo ya uchumi na jamii wanaamini kuongezeka kwa furaha ya wananchi kwa ujumla wao ndiyo kipimo mahususi cha maendeleo ya uchumi wa jamii.

"Mambo muhimu yanayowafanya wananchi kuwa na furaha ni pamoja na jamii inayojaliana, uhuru, ukarimu, kuaminiana, afya njema, kipato kizuri na utawala bora. Tangu mwaka 2012, taarifa ya furaha duniani hutolewa ambapo mwaka 2020 Tanzania imekuwa nchi ya 148 isiyokuwa na furaha kati ya nchi 153 duniani kote," alisema.

Profesa Lipumba alisema katiba ya sasa haikidhi maendeleo ya demokrasia nchini, hivyo chini ya sera yao ya haki sawa na furaha kwa wote, serikali ya umoja wa kitaifa watakayoiunda, itaandaa utaratibu unaofaa wa kupata katiba mpya ya wananchi yenye misingi ya demokrasia kwa kuzingatia rasimu ya Tume ya Jaji Warioba.

Profesa Lipumba alisema serikali ya CUF itahakikisha watoto wote wa Tanzania wana haki ya kupata elimu bora ya msingi, sekondari na elimu ya juu na kila raia ajiendeleze kielimu hasa kwa kutumia vizuri teknolojia ya habari na mawasiliano.

"Serikali itakayoundwa na CUF chini ya dira ya mabadiliko, itatoa kipaumbele maalumu katika kuwaendeleza kielimu wasichana na kujenga misingi imara ya kuendeleza elimu ya hisabati, sayansi na teknolojia," Profesa Lipumba alisema.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza, aliyehudhuria mkutano huo, alikipongeza chama hicho kwa kufanya siasa za kisomi na zisizokuwa na matusi na kueleza kuwa hali hiyo inaonyesha dhahiri kuwa kipo imara.

Alikishukuru chama hicho kwa kusimama imara wakati wa mapambano dhidi ya corona na kuungana na Rais Magufuli katika kuhakikisha nchi inaondoka katika taharuki ya ugonjwa huo.

"Ninawapongeza sana kwa kuahidi kufanya kampeni za kistaarabu katika uchaguzi huu kwa kuzingatia maslahi ya taifa," alisema na kuahidi kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inawaasa wafuate sheria za nchi katika kutafuta ushindi kwenye uchaguzi mkuu na si vinginevyo.

Alikumbusha kuwa mwaka 1996, Rais mstaafu Benjamini Mkapa, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia Ijumaa, alianza kutoka ruzuku kwa vyama vya siasa na CUF walikuwa miongoni mwa vyama vilivyonufaika na ruzuku hiyo.

Nyahoza pia alikumbusha kuwa, ni katika kipindi cha uongozi wa Mkapa, nafasi za viti maalum zilianzishwa kwa lengo la kuwainua wanawake, kundi ambalo lilikuwa limeachwa nyuma katika vyombo vya uamuzi.

## HABARI KITAIFA

# NEC yawafunda wasimamizi wa uchaguzi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC),imewataka wasimamizi wa Uchaguzi Mkuu mwaka huu, kuepuka kufanya kazi kwa mazoea ili kuondoa malalamiko yanayojitokeza wakati wa uchaguzi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mjumbe wa Tume hiyo, Omari Ramadhan Mapuri, alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tatu jijini hapa yaliyokutanisha washiriki 162 Kanda ya Kati.

"Uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu mbalimbali zinazopaswa kufuatwa na kuzingatiwa, fuateni hatua na taratibu hizi ndiyo msingi wa uchaguzi mzuri wenye ufanisi usio na malalamiko," alisema.

Mapuri aliwataka wasimamizi hao kubadilishana uzoefu, kujadili namna bora ya kufanikisha uchaguzi.

"Pia kujadili namna bora ya kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika hatua mbalimbali za uchaguzi, Kafanyeni kazi kwa kufuata maadili kwa kuzingatia sheria, kanuni pamoja na maagizo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Uchaguzi," alisema.

Mapuri alisema wasimamizi hao wameaminiwa na kuteuliwa na Tume katika nafasi hizo za usimamizi wa uchaguzi kwa kuwa wana uwezo wa kufanya kazi hiyo hivyo wanatakiwa wajiamini na kujitambua.

Alitoa wito kwa wasimamizi hao kuhakikisha kuwa wanayaelewa vema maeneo yao ya kazi kijiografia na kuhakikisha kwamba wanawatumia vizuri wasaidizi walio chini yao katika maeneo yao ili kutoa matokeo bora.

"Tambueni miundombinu mbalimbali ya kufika kwenye vituo vya kupigia kura katika majimbo wanayosimamia uchaguzi," alisema.

Mapuri aliwasisitiza washirikishane na vyama vya siasa pamoja na wadau wengine wa uchaguzi katika mstakabali mzima wa uchaguzi ili kuongeza uwazi katika uchaguzi na hivyo kuleta ufanisi.

Katika mafunzo hayo, wapo wasimamizi 24, wasimamizi wasaidizi uchaguzi katika majimbo wapo 87, maofisa uchaguzi 24, waratibu wa uchaguzi watatu na maofisa ugavi 24 ambapo kati yao, 55 wanatoka mikoa ya Dodoma, Morogoro 61 na Singida 46.

Awali, wasimamizi walikula kiapo cha utii kilichoongozwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi Wilaya ya Dodoma, Mary Senapee, ambaye aliwataka washiriki hao kusaini baada ya kuapa kwani wakikiuka maadili ya uchaguzi ndicho kitakachowafunga.

## WADAU UHIFADHI WAOMBWA KUWALINDA WANYAMAPORI

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imewaomba wadau wa uhifadhi nchini kushirikiana na mamlaka katika kuhifadhi kwa kuwalinda wanyamapori kwa maslahi ya Taifa.

Kamishna Mhifadhi wa TAWA ,Mabula Misungwi, alisema hayo jana wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa Utali katika kikao cha kupitia mkakati wa huduma za ujirani mwema wa uhifadhi kilichofanyika katika makao makuu ya mamlaka mamlaka hiyo Mjini Morogoro.

Misungwi alisema, TAWA imekuwa ikichangia miradi mingi ya kimaendeleo kwa jamii inayozunguka maeneo yanayohifadhiwa na mamlaka hiyo kupitia utalii wa picha na uwindaji wa kitalii.

Aidha, Misungwi alisisitiza haja ya kuweka mpango wa kushirikiana katika kudhibiti wanyamapori waharibifu nchini ili kuleta tija ya uhifadhi.

Alisema TAWA imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha jamii inanufaika na uhifadhi kwa maeneo wanayowazunguka kwa kusaidia miradi ya maendeleo ikiwamo afya, elimu na huduma ya majisafi na salama.

Nae Gloria Bideberi, msimamizi wa kitengo cha Ujirani Mwema wa TAWA, alisema fedha zilizotumwa na wadau wa utalii kwa kipindi cha mwaka 2017-2020 ni Sh. bilioni 4 ambazo ni fedha za Kitanzania zilizotumika katika maendeleo ya jamii.

Akizungumzia changamoto, Bideberi alisema wanakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kama vile magari na sare za askari wa vijiji.

Nao baadhi ya wadau wa TAWA, wameitaka mamlaka hiyo kushirikiana katika kukabiliana na wanyamapori waharibifu wa mazao, pia kusaidia manunuzi ya vitendea kazi kama mavazi na magari.

Kikao kazi hicho kimehusisha wadau mbalimbali wa uhifadhi kama halmashauri za wilaya, wadau wa maendeleo, mashirika ya uhifadhi, vyuo na watoa huduma za utalii.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII



Benjamin William Mkapa
(1938 - 2020)

SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Kamati ya Taifa ya Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF tunaungana na Watanzania wote kumpa pole **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Joseph Magufuli , familia na Watanzania** wote kwa kifo cha **Rais wa Awamu ya Tatu wa Tanzania, Mhe. Benjamin William Mkapa.**

Daima tutamkumbuka kwa mchango wake katika kupambana na umaskini.

*Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amen*

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
S.L.P. 2719 Dodoma, Tanzania
Simu: **+255 26 296 3866** Nukushi: +255 26 296 3871
Tovuti: **www.tasaf.go.tz** Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Mzee Mkapa ametuachia mengi ya kumkumbuka*

**TANGU** Rais John Magufuli alipotangaza msiba wa Taifa wa Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Mzee Benjamin Mkapa, Ijumaa iliyopita, Watanzania wengi wamepata majonzi, simanzi na masikitiko.

Watu mbalimbali, wakiwamo waliokwenda kutoa pole kwa familia Masaki jijini Dar es Salaam, waombolezaji wanaoendelea kujitokeza katika Uwanja wa Uhuru kwa ajili ya kuaga mwili, Watanzania walioko ughaibuni pamoja na jumuiya ya kimataifa, wamemuelezea Mzee Mkapa jinsi gani alivyoishi wakati wa uhai wake na mambo mengi mazuri aliyoyafanya.

Mkapa ameelezewa hasa katika mchango wake alioutoa kwa taifa lake kwa kulitumikia kwa uaminifu, uadilifu, uzalendo huku akielezewa kwa kujali, kuthamini na kutanguliza mbele maslahi ya waafrika na uafrika wakati wote wa maisha yake ya uongozi.

Kimsingi, mambo mengi yameelezewa kuhusu maisha ya kiongozi huyo na mambo aliyoyafanyia nchi yake, Afrika na duniani kwa ujumla, lakini tunapenda kuweka msisitizo na kuishauri jamii iendelee kuyakumbuka na kuyaendeleza mambo yote mazuri ya Hayati Mzee Mkapa.

Kwa upande wa eneo la kusuluhisha migogoro ambalo Mkapa alitumia muda mrefu wa maisha yake kulishughulikia, tunashauri kwamba viongozi wetu walioko madarakani na wastaafu kuliendeleza jambo hili kwa lengo la kuzisaidia nchi nyingi hususan za bara hili ambazo bado zinakabiliwa na mizozo na nyingine ambazo zitatumbukia huko.

Mkapa akiwa Waziri wa Mambo ya Nje alishughulikia migogoro mbalimbali pale alipokuwa akitumwa na marais wake kwa vipindi tofauti Mwalimu Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi.

Mzee Mkapa pia baada ya kustaafu aliendeleza juhudi za upatanishi katika maeneo mbalimbali yakiwamo Burundi, Sudan Kusini kupitia Umoja wa Mataifa (UN) ambako alisimamia kura ya maoni iliyoamua taifa hicho changa zaidi duniani kujitenga kutoka Sudan.

Kadhalika, alikuwa katika jopo lililoteuliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa UN, Ban Ki-moon kusuluhisha machafuko yaliyoibuka Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 na kusababisha vifo vya watu takribani 500 na wengine takribani 1,500,000 kupoteza makazi.

Atakumbukwa pia kwa jinsi alivyozungumzia ngazi ya kimataifa na kutetea ukombozi wa nchi za afrika ambazo zilikendelea kutawaliwa katika miaka ya 1980 na 1960 za Zimbabwe, Namibia pamoja na harakati za kuondoa siasa ya ubaguzi wa rangi Afrika Kusini iliyokuwa imehalalishwa kisheria na utawala wa makaburu dhidi ya weusi.

Wakati wa vita ya Tanzania dhidi ya utawala wa Iddi Amini wa Uganda, Mkapa alikuwa Waziri wa mambo ya Nje, na kwa hakika alipigana vita ya kidiplomasia kutokana na aliyvyoelezea msimamo wa Tanzania katika vikao vya uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) na kwenye vikao vya UN, na wakati mwingine kutumia lugha kali.

Hakika ufafanuzi alioufanya Mkapa alipokuwa akitumwa na Mwalimu Nyerere kuelezea sababu za Tanzania kuendelea na vita hiyo licha ya jitihada za kupatanishwa, ulieleweka kwa waliokuwa wanailaumu Tanzania kukataa kusitisha vita.

Ujasiri huo unapaswa kutuachia funzo kwamba wanaopewa dhamana ya uongozi hususan katika eneo la diplomasia hawanabudi kutekeleza majukumu yao ikiwamo kuzungumza katika majukwaa ya kimataifa bila woga wala aibu hususan pale inapotokea maslahi ya taifa kuhatarishwa .

Kuboreshwa kwa huduma za jamii kama elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara na zingine, kulichangiwa na jitihada za Mkapa kuweka msingi imara wa makusanyo ya kodi baada ya kuanzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mkapa pia ataendelea kukumbukwa kwa ubunifu wake katika kupunguzia wananchi umaskini kupitia kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) pamoja na Mkakati wa Kurasimisha Mali za Wanyonge (MKURABITA).


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



# Mkapa kaondoka, kaacha zawadi ya kudumu ni sekondari za kata

**Na Sabato Kasika**

TANGU mwishoni mwa wiki iliyopita, Watanzania wako ndani ya lindi la majonzi, wakiomboleza kumpoteza mstaafu Benjamin Mkapa, aliyeongoza taifa katika awamu ya tatu.

Kuna mengi mazuri yamezungumzwa na kutajwa, nikiri si rahisi kuweka hesabu la kila alichofanya hadharani. Ila, kuna la kipekee ambalo linaheshimika hasa na wazazi, walezi na vijana wao nalo ni ujenzi wa sekondari za kata.

Mkapa alipoingia madarakani katika awamu yake, aliendeleza sekondari za kata ikiwa ni sehemu ya mipango yake, hapana shaka, alikuwa anatekeleza anachokijua kwa maana elimu ya msingi ilishakomaa kwa kiasi kikubwa; kila kijiji, na kitongoji.

Sekondari za kata zilijengwa kwa nguvu za wananchi wenyewe serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Mkapa ikihamasisha kila kata nchini nzima kuwe na sekondari wakati huo Waziri wa Elimu akiwa Joseph Mungai.

Kikosi kiliteuliwa kila mkoa, wakuu wa mikoa waliagizwa kuhamasisha ujenzi huo na sasa matunda yanaonekana kwani baadhi ya shule zimetoa wanafunzi waliokwenda kidato cha tano na hata vyuo vikuu.

Tukumbuke kwamba ilianzishwa 'mafunzo ya muda mfupi au 'crash program' iliyolenga kuongeza idadi ya walimu nchini ikachukua wanafunzi waliomaliza kidato cha nne na kuwapeleka vyuoni kwa mwaka mmoja na wale wa sekondari waliopata mafunzo ya miezi mitatu ili kuziba pengo la uchache wa walimu.

> **Ujenzi wa sekondari hizo umeendelezwa na awamu ya nne na sasa ya tano kwa kutumia nguvu za wananchi ambazo kimsingi shule hizo ni mali yao na wanatakiwa kuzitunza na kuziendeleza.**

Itoshe kusema Mkapa ameondoka, lakini kwa upande wa elimu, ameacha zawadi ya kudumu ambayo ni sekondari, ingawa awali zilibezwa na baadhi ya watu, huku wakizipachika majina mbalimbali ya kukebehi.

Ujenzi wa sekondari hizo umeendelezwa na awamu ya nne na sasa ya tano kwa kutumia nguvu za wananchi ambazo kimsingi shule hizo ni mali yao na wanatakiwa kuzitunza na kuziendeleza.

Ikumbukwe kwamba wakati Rais Mkapa hajamaliza muda wake wa uongozi alifungua shule nyingi za kata nchi nzima zikiwamo zilizowekewa jiwe la msingi na sasa zinaendelea kufanya kazi.

Katika utaratibu wa kupokezana vijiti, hicho awamu ya nne, iliyoongozwa na Jakaya Kikwete na timu yake walirithi jukumu hilo walipoanza kazi, kwani moja ya majukumu yao ilikuwa ni kuboresha sekondari za kata.

Hapo ndipo Waziri Mkuu wa awamu hiyo Edward Lowasa, alifanya mageuzi makubwa na maboresho ya sekondari hizo nchini ambazo waliachiwa na serikali ya awamu ya tatu.

Aidha, awamu hiyo iliwekeza katika kujenga maabara za shule hizo na kuzipa vifaa ili kuziimarisha kitaaluma zaidi.

Sasa serikali ya awamu ya tano nayo inaendeleza sekondari hizo ikiwamo pia kujenga nyingine zaidi ikiwa sasa imefikia baadhi ya wazazi kujenga sekondari za vijiji vyao badala ya kata.

Hadi kufikia kujenga sekondari ya kijiji, ni wazi kuna hatua nzuri ambazo zimepigwa katika maendeleo ya elimu nchini, ambayo yalikolezwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ya Hayati Benjamin Mkapa.

# Wadadisi watakiwa kutoa takwimu sahihi za kilimo

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

WADADISI wa sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka wa kilimo 2019/20 wametakiwa kuhakikisha takwimu watakazotoa ziwe kweli ili kuiwezesha serikali kupanga sera, mipango mbalimbali ya kuwaendeleza, kuimarisha kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wananchi.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Peres Magiri, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wadadisi wa sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka wa kilimo kwa mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma, Katavi na Singida.

Alisema sensa hiyo ni muhimu kwa kuwa ina lengo la kufahamu hali halisi ya kilimo, ufugaji na shughuli za uvuvi kwa kuwa na takwimu zitakazoonyesha hali halisi ya sekta hizo nchini ambazo zitatumika kufuatilia viashiria vya Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030.

Magiri alisema ni muhimu kuwa na mipango ambayo itasaidia katika kutokomeza njaa kwa kuwa na uhakika wa chakula kupitia ukuzaji wa kukuza kilimo.

Aliwataka wananchi hadi viongozi katika mikoa yote kuipa uzito sensa hiyo kwa kuhakikisha inafanyika kwa ufanisi ili itoe matokeo tarajiwa.

Magiri alisema kilimo ni muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi ambapo kwa mwaka 2019, kilimo kilichangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 26.6, na kwa upande wa mauzo ya nje asilimia 24.3 ya fedha za kigeni zilizopatikana zilitokana na mazao ya kilimo.

Aidha, aliwataka wadadisi kuhakikisha watumia mbinu walizofundishwa na nyingine za ubunifu kupata takwimu sahihi hasa kwenye jamii za wafugaji, ambao mara nyingine hawapendi kutaja idadi halisi ya mifugo yao.

Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Philemon Mwenda, aliwataka wadadisi kufanyakazi kwa bidii na maarifa na hususani jinsi kutumia ya vishikwambi katika kukusanya takwimu husika.

Alisema kutakuwapo na usimamizi wa karibu na kama itabainika mdadisi yeyote anakiuka maadili ya ukusanyaji wa takwimu hizo kwa wakuu wa kaya sheria, itachukua mkondo wake ipasavyo.

Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Mussa Hussein, alisema ni vema wadadisi waliopewa jukumu hilo za kukusanya takwimu katika ngazi ya halmashauri kuhakikisha zinakuwa halisi na sio za kutengeneza.

Alisema kumekuwapo na kasoro nyingi pindi Ofisi ya Mkoa inapotaka takwimu unakuta zilizotolewa jana zinatofautiana na siku zinazofuata na kuonyesha kuwa hawako makini.

## TBS yawanoa wajasiriamali ubora bidhaa

**Na Mwandishi Wetu, BUKOBA**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limeendesha mafunzo maalumu ya ujasiriamali na umuhimu wa ubora wa bidhaa kwa wajasiriamali mkoani Kagera kwa lengo la kuboresha bidhaa zao na kuendana na ushindani katika soko la dunia.

Mafunzo hayo yalifanyika jana katika ukumbi wa hoteli ya Bukoba yakiwashirikisha zaidi ya wajasiriamali 50 kutoka wilaya za mkoa huo.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawiro, alilishukuru shirika hilo kwa kuwafikia wajasiriamali kwenye maeneo yao na kuweza kuzijua changamoto zao katika usindikaji wa bidhaa zao.

Kinawiro amesema kuwa wajasiriamali ni watu muhimu katika ukuaji wa uchumi wa taifa ambao wanatakiwa kusaidiwa kwa kupewa elimu ya ujasiriamali na utunzaji wa bidhaa tangu zikiwa malighafi hadi hatua ya kwenda sokoni.

"Wajasiriamali ni watu muhimu kwa taifa letu. TBS mna jukumu kubwa la kuhakikisha wadau hawa wanapata elimu sahihi na bora yenye lengo la kuwainua katika shughuli zao. Nchi yetu imefikia uchumi wa kati na mchango wa watu hawa upo mkubwa," alisema.

Kinawiro alisema mkoa wa Kagera unapakana na nchi takribani nne ambazo zinaweza kuwa fursa kwa wajasiriamali wa mkoa huo, hivyo wakikosa alama za ubora kwenye bidhaa zao watakosa masoko katika nchi hizo kwa kuwa zitakuwa hazitambuliki hata kama ni nzuri.

Mkuu huyo wa wilaya pia alizitaka TBS na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na TBS kuwasaidia wajasiriamali kupata vifungashio bora ili kuuza bidhaa zao kwa usafi na ubora na pia kupata faida. Alisema changamoto hiyo imekuwa kero na kuwafanya wajasiriamali kutumia vifungashio visivyo bora na kusababisha watumiaji kushindwa kununua bidhaa zao.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY
ISO 9001:2015 CERTIFIED



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) tumepokea kwa masikitiko makubwa ya taarifa za kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

**Mhe. Benjamin William Mkapa.**

Tunatoa pole kwa Familia, Ndugu, Jamaa, Marafiki na Watanzania wote.

***PUMZIKA KWA AMANI.***



**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**
**Mawasiliano Towers**
**20 Barabara ya Sam Nujoma**
**S.L.P 474/14414 Dar es salaam,Tanzania**
**Barua pepe: dg@tcra.go.tz/www.tcra.go.tz**

# TANGAZO

EXIM AT WORK TODAY FOR TOMORROW

## "EXIM AT WORK TODAY, FOR TOMORROW"

EXIM AT WORK TODAY FOR TOMORROW

## EXIM BANK (TANZANIA) UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA AMBAZO HAZIJAKAGULIWA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014.

Fedha za Wanahisa @TZS 165 Bilioni

Jumla ya Mali @ Trilioni 1.8

Amana za Wateja @ Trilioni 1.34

Matawi @ 48

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2020 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KAMPUNI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2020 | KUNDI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2020 | KAMPUNI ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2020 | KUNDI ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| A | MALI | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 40,068 | 62,796 | 28,040 | 50,011 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 108,888 | 205,740 | 59,379 | 140,126 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 199,691 | 204,021 | 215,215 | 219,798 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 31,550 | 92,903 | 65,291 | 142,395 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 1,362 | 3,463 | 1,340 | 2,676 |
| 6 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 27,460 | 27,625 | 32,280 | 56,487 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyigine | 6,731 | 38,172 | 7,061 | 31,871 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 714,811 | 983,020 | 700,610 | 962,072 |
| 12 | Mali nyingine | 41,269 | 57,934 | 41,482 | 58,099 |
| 13 | Uwekezaji katika Hisa | 36,812 | 2,731 | 35,931 | 5 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 57,098 | 76,500 | 58,620 | 72,643 |
| 16 | Mali isiyo ya sasa yanayotumiwa | 15,949 | 17,862 | 15,949 | 17,862 |
| **17** | **JUMLA YA MALI** | **1,281,688** | **1,772,767** | **1,261,197** | **1,754,043** |
| B | DHIMA | | | | |
| 18 | Amana za Benki na Taasisi za Fedha | 166,444 | 29,950 | 206,948 | 58,403 |
| 19 | Amana za Wateja | 763,318 | 1,339,038 | 707,186 | 1,299,290 |
| 20 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| 21 | Amana Maalumu | 20,723 | 20,723 | 10,479 | 10,479 |
| 22 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 281 | 281 | 1,163 | 1,163 |
| 23 | Hundi na Hawala za Kibenk Zilitolewa | 1,496 | 4,039 | 1,562 | 3,567 |
| 24 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 8,603 | 11,434 | 8,566 | 11,876 |
| 25 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya benki | - | - | - | - |
| 26 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 27 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 2,037 | 2,231 | 1,616 | 2,018 |
| 28 | Dhima Nyingine | 45,683 | 74,151 | 41,296 | 67,195 |
| 29 | Madeni | 125,210 | 125,636 | 138,527 | 138,693 |
| **30** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,133,793** | **1,607,483** | **1,117,342** | **1,592,685** |
| **31** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **147,895** | **165,284** | **143,856** | **161,358** |
| C | FEDHA ZA WANAHISA | | | | |
| 32 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 12,900 | 12,900 | 12,900 | 12,900 |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 24,810 | 32,537 | 37,996 | 45,234 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | 104,224 | 102,812 | 91,146 | 89,527 |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 5,961 | 7,288 | 1,814 | 3,225 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - | - | - |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | 9,747 | - | 10,472 |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **147,895** | **165,284** | **143,856** | **161,358** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | 190,668 | 192,317 | 195,414 | 198,264 |
| 40 | Mikopo Chechefu | 124,985 | 151,242 | 174,673 | 204,590 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 56,963 | 72,078 | 59,292 | 66,551 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | 4,117 | 4,117 | 4,117 | 4,117 |
| D | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | | | |
| | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.54% | 8.77% | 11.41% | 8.60% |
| | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 16.14% | 14.28% | 22.93% | 19.82% |
| | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 83.30% | 77.36% | 83.32% | 76.04% |
| | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.77% | 55.45% | 55.55% | 54.85% |
| | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.35% | 76.07% | 83.76% | 80.54% |
| | Ongezeko la Amana | 2.80% | 0.83% | -7.08% | -2.83% |
| | Ongezeko la Mali | 1.62% | 1.07% | -6.27% | -1.80% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2020 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KAMPUNI ROBO YA MWAKA YA SASA 30.06.2020 | KUNDI ROBO YA MWAKA YA SASA 30.06.2020 | KAMPUNI ROBO YA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2019 | KUNDI ROBO YA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2019 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2020 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2020 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2019 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 24,834 | 32,482 | 26,356 | 34,546 | 50,695 | 66,878 | 49,885 | 64,420 |
| 2 | Gharama za Riba | (9,038) | (10,313) | (8,463) | (10,580) | (18,474) | (21,865) | (16,127) | (18,797) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **15,796** | **22,169** | **17,894** | **23,967** | **32,221** | **45,012** | **33,758** | **45,623** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (21) | (21) | (220) | (220) | - | - | (353) | (353) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 5,410 | 4,836 | (1,716) | (2,686) | 4,423 | 2,447 | (2,921) | (4,590) |
| 6 | Mapato Yasiyo ya Riba: | 7,864 | 12,504 | 7,532 | 13,669 | 16,782 | 27,924 | 17,134 | 26,677 |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,924 | 3,167 | 1,921 | 3,151 | 3,795 | 6,875 | 5,434 | 7,960 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 3,630 | 7,402 | 4,852 | 8,634 | 9,041 | 17,684 | 9,856 | 17,106 |
| | 6.3 Gawio | 311 | 11 | 21 | 21 | 411 | 11 | 21 | 21 |
| | **6.4 Mapato Mengine** | **1,999** | **1,923** | **738** | **1,864** | **3,534** | **3,354** | **1,825** | **1,590** |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(23,259)** | **(32,908)** | **(20,553)** | **(29,169)** | **(45,086)** | **(63,934)** | **(41,622)** | **(56,542)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (8,886) | (13,467) | (8,479) | (12,698) | (17,903) | (27,192) | (16,816) | (24,825) |
| | **7.2 Ada na Kamisheni** | **31** | **(398)** | - | **(445)** | - | **(850)** | - | **(683)** |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (14,404) | (19,042) | (12,074) | (16,026) | (27,184) | (35,891) | (24,807) | (31,033) |
| 8 | Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 5,791 | 6,580 | 2,937 | 5,561 | 8,339 | 11,449 | 5,996 | 10,815 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (1,644) | (2,480) | (490) | (1,249) | (2,378) | (4,161) | (1,408) | (3,090) |
| 10 | Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 4,147 | 4,100 | 2,447 | 4,313 | 5,961 | 7,288 | 4,588 | 7,725 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyo-jumuishwa (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | 4,147 | 4,100 | 2,447 | 4,313 | 5,961 | 7,288 | 4,588 | 7,725 |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 708 | 1,046 | 675 | 970 | 708 | 1,046 | 675 | 970 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 462 | 318 | 190 | 334 | 462 | 565 | 356 | 599 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 33 | 48 | 32 | 46 | 33 | 48 | 32 | 46 |
| | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | | | | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.3% | 0.8% | 0.8% | 1.0% | 0.9% | 0.7% | 0.5% | 0.6% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 11.0% | 7.7% | 5.3% | 7.1% | 7.9% | 6.9% | 3.3% | 4.3% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 80.1% | 83.3% | 80.8% | 77.5% | 84.4% | 84.8% | 81.8% | 78.2% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.1% | 5.6% | 7.2% | 6.7% | 6.2% | 5.7% | 4.6% | 4.2% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.06.2020 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KAMPUNI ROBO YA MWAKA SASA 30.06.2020 | KUNDI ROBO YA MWAKA SASA 30.06.2020 | KAMPUNI ROBO MWAKA ILIYOPITA 30.06.2019 | KUNDI ROBO MWAKA ILIYOPITA 30.06.2019 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2020 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2020 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.06.2019 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.06.2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **5,791** | **6,580** | **2,548** | **4,911** | **8,339** | **11,449** | **5,996** | **10,815** |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | (3,124) | (5,118) | 3,445 | 3,828 | 1,780 | (1,289) | 7,732 | 1,527 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (14,201) | (20,947) | 8,135 | (8,698) | (6,066) | (29,646) | (7,948) | (45,524) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | 425 | 425 |
| | Net Gain/Loss on disposal of AFS | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 25,872 | 21,538 | (70,416) | (80,262) | (44,544) | (58,723) | 44,223 | 81,208 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,307 | 6,342 | (10,115) | (559) | (6,809) | 5,789 | (1,176) | 5,744 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,713 | 143 | (502) | (13,777) | 1,211 | (13,635) | (4,857) | (11,732) |
| | Non-current assets held for sale | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Kodi Iliyolipwa | (1,027) | (1,027) | (1,027) | (1,027) | (2,054) | (2,054) | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **18,331** | **7,510** | **(67,932)** | **(95,584)** | **(48,142)** | **(88,109)** | **44,395** | **42,464** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | 21 | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,510) | (1,510) | (746) | (1,096) | (2,255) | (2,569) | 966 | (3,405) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | (425) | (425) |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (24,942) | (31,322) | 31,357 | 70,608 | 4,956 | 39,286 | (34,888) | (68,825) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(26,452)** | **(32,832)** | **30,611** | **69,512** | **2,701** | **36,716** | **(34,327)** | **(72,654)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (13,317) | (13,057) | (5,693) | (5,527) | (19,010) | (18,584) | 19,020 | 19,720 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(13,317)** | **(13,057)** | **(5,693)** | **(5,527)** | **(19,010)** | **(18,584)** | **19,020** | **19,720** |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(21,438)** | **(38,378)** | **(43,014)** | **(31,598)** | **(64,451)** | **(69,977)** | **29,089** | **(10,471)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **191,585** | **353,532** | **234,599** | **385,130** | **234,599** | **385,130** | **198,704** | **296,452** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **170,147** | **315,153** | **191,585** | **353,532** | **170,147** | **315,153** | **227,794** | **285,980** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2020 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| KAMPUNI | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | "Mengineyo (bainisha)" | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **91,187** | **37,385** | **-** | **611** | **142,084** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 5,961 | - | - | - | 5,961 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 13,037 | (13,037) | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (150) | (150) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | **-** | **110,185** | **24,348** | **-** | **462** | **147,895** |
| **Mwaka Uliopita** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 12,900 | - | 135,452 | 4,488 | 6,402 | (13) | 159,229 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,769) | - | - | - | (17,769) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 624 | 624 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| **Ziada ya Kisheria** | **-** | **-** | **(32,897)** | **32,897** | **-** | **-** | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 6,402 | - | (6,402) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | **-** | **91,187** | **37,385** | **-** | **611** | **142,084** |

| KUNDI | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | "Mengineyo (bainisha)" | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **88,712** | **41,762** | **3,812** | **10,943** | **158,129** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 8,351 | - | - | (1,064) | 7,288 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 13,037 | (13,037) | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (132) | (132) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | **-** | **110,100** | **28,725** | **3,812** | **9,747** | **165,284** |
| Mwaka Uliopita | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **129,227** | **8,865** | **6,290** | **9,167** | **166,449** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (13,814) | - | - | (1,179) | (14,993) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | 3,812 | (3) | 3,809 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | 2,863 | 2,863 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (32,897) | 32,897 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 6,196 | - | (6,290) | 95 | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | **-** | **88,712** | **41,762** | **3,812** | **10,943** | **158,129** |

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| JAFFARI MATUNDU **OFISA MTENDAJI MKUU** | ................................... | **27.07.2020** |
| SHANI KINSWAGA **MKUU WA FEDHA** | ................................... | **27.07.2020** |
| COLMAN RIWA **MKAGUZI MKUU WA NDANI** | ................................... | **27.07.2020** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| YOGESH MANEK **MKURUGENZI** | ................................... | **27.07.2020** |
| BALOZI JUMA MWAPACHU **MKURUGENZI** | ................................... | **27.07.2020** |

Kwa maelezo zaidi piga simu 080 078 0111 au tembelea visit www.eximbank.co.tz

EXIM BANK *Innovation is life*

TANGAZO

# EXIM BANK (TANZANIA) LIMITED MINIMUM DISCLOSURE OF THE BANK CHARGES AND FEES FOR THE ENDED 30TH JUNE 2020

| BANK SERVICE | CHARGE/FEE |
|---|---|
| **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| Transaction fee | N/A |
| Monthly service fee ( break down per customer type) | 4000 |
| Annual Fee (Student Account) | 10000 |
| Statement | FREE |
| Interim statement | 6000 |
| Withdrawal Charges at domicile branch | 3500 |
| Withdrawal Charges over the Counter at non domile branch for non preferred customers | 1.2% of the amount |
| Withdrawal bulky without notice | N/A |
| Cash Deposit Charge at Domicile branch | FREE |
| Cash Deposit Charge at non domicile branch by non preferred customers | FREE |
| Savings Card/Passbook | N/A |
| Passbook/Card Replacement | N/A |
| Coin Deposit Fee | 12% of the amount |
| Closing Account | FREE |
| | |
| **CURRENT ACCOUNT** | |
| Monthly service fee ( break down per customer type) | 18000 |
| Transaction fee | N/A |
| Statement | FREE |
| Interim statement | 6000 |
| Periodic Schedule Statement | N/A |
| Withdrawal Charges at domicile branch | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject ot maximum of 125,000 |
| Withdrawal Charges over the Counter at non domile branch for non preferred customers | 1.2% of amount |
| Cash Deposit Charge at domicile branch | FREE |
| Cash Deposit Charge at non domicile branch by non preferred customers | FREE |
| Coin Deposit Fee | 12% of the amount |
| Closing Account | FREE |
| Deposit fee | N/A |
| Bank Drafts | N/A |
| Bank Drafts cancellation charge | N/A |
| Cheque book | 60,000 for 100 leaves and 42,000 for 50 leaves |
| Inward Cheque Clearing | 1000 |
| Cash Withdrawal at Counter | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject ot maximum of 125,000 |
| Special Clearance | N/A |
| Cheque withdraw over the counter | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject ot maximum of 125,000 |
| Dishonoured cheque | 30000 |
| Cash Payment to 3rd party | FREE |
| Cash Deposit Charge | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject ot maximum of 125,000 |
| Overdrawn account interest charge | 27% of the amount overdrawn |
| Unarranged Overdraft | N/A |
| Bulk cash Deposit | N/A |
| Bulk cash Withdrawal | N/A |
| Stop Payment orders | 42000 |
| Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| Standing Orders ( to other bank) | 30000 + Tiss charges |
| Certificate of Balance | 15000 |
| Letter of introduction | FREE |
| Salary handling | FREE |
| School fees deposits | FREE |
| TRA collection | FREE |
| Safe custody charges | Small: 180,000 Medium:270,000 Large:720,000 and Extra large 840,000 p.a |
| Safe custody access fees | FREE |
| | |
| **EFT** | |
| Within the same bank (On Us) | 1200 |
| To other Banks ( On Others) | 1200 |
| | |
| Outward Transfers | USD 60 |
| Inward foreing Transfers(foreing inward remittances) | USD 6 for receipt up to USD 10k AND USD 12 for receipt above USD 10K |
| | |
| **TISS** | |
| Within the same bank (On Us) | FREE |
| To other Banks ( On Others) | 10,000 per entry |
| | |
| **FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT** | **Savings Acc** |
| Transaction fee | N/A |
| Statement | FREE |
| Interim statement | N/A |
| Withdrawal Charges at domicile branch | 1.44% of amount |
| Withdrawal Charge of Low denomination notes of (20,10,5, and 1) | FREE |
| Withdrawal Charges over the Counter at non domile branch for non preferred customers | 2.4% of amount |
| Cash Deposit Charge at domicile branch | 12% for small Denominations (1,5,10,20) only |
| Cash Deposit Charge at non domicile branch by non preferred customers | FREE |
| Cash Deposit charge of low denomination notes of (20,10,5, and 1) | 12% of amount |
| Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A |
| Purchase of Foreign Cheque | N/A |
| Sale/ Purchase of cash passport | N/A |
| Telex/SWIFT | N/A |
| Transfer from foreign currency denominated account to local account | FREE |
| Outward foreign transfers | 60USD/42GBP/42EUR/600ZAR |
| Inward foreign transfers - Customers | |
| LC Opening/ Advising commision (cash covered) | 1.8%p.a(Negotiable for large amounts) Min $600+$240 swift charges |
| LC Opening/ Advising commision (No cash covered) | 180 USD |
| LC Acceptance commission | N/A |
| LC Payment/settlement commision | N/A |
| LC Amendments | 120 USD |
| Others | NIL |
| | |
| **ATM TRANSACTIONS** | |
| Local Cards | |
| Issue of ATM card | N/A |
| Replacement ATM Card (Faulty) | N/A |
| Replacement ATM Card (Lost) | N/A |
| | |
| International Cards | |
| Issue of ATM card | FREE |
| Issue of Prepaid Card | Tzs 10,000 |
| Balance Inquiry – onus ATM | 240 |
| Balance Inquiry – Remote onus ATM | 600 |
| PIN regeneration | 6600 |
| ATM card replacement(Faulty/Lost) | 19000 |
| EMV Annual fee | Tzs 2,000/ 1000(Student EMV fee) per month |
| | |
| **ATM WITHDRAWALS:** | |
| Within the same bank (On Us) | 1200 per transaction |
| To other banks ATM (On others) | 3.6% of withdrawal, Min Tsh 2200 |
| ATM mini statement | 400 |
| Bill payments through ATM | N/A |
| | |
| **POS** | |
| Within the same bank (On Us) | FREE |
| To other banks ATM (On others) | FREE |
| | |
| **MOBILE (SMS) BANKING** | |
| Balance Inquiry | 240 |
| Payments | As per service provider tariff |
| Transfers | Tzs 1,200-Tzs 6,000 |
| | |
| Mini Statement | 240 |
| **INTERNET BANKING** | |
| Domestic: | N/A |
| Balance Inquiry | N/A |
| Payments | N/A |
| | |
| International | |
| Balance Inquiry | 7200 per annum |
| Payments | Tsh 600 per month for Individual & Tsh 15,000 per month for Corporate |
| Transfers | Token Fee of Tsh 100,000 |
| | |
| **MONEY REMITTANCES** | |
| Western Union | N/A |
| Sending | N/A |
| Received | N/A |
| | |
| Money Gram | |
| Inward | FREE |
| Outward | As per Moneygram tariff |
| | |
| Coinstar | |
| Inward | N/A |
| Outward | N/A |

| | |
|---|---|
| **Travelex** | |
| Inward | N/A |
| Outward | N/A |
| | |
| Africash | |
| Inward | N/A |
| Outward | N/A |
| | |
| Others (Specify) | |
| Inward | NIL |
| Outward | NIL |
| | |
| **Credit card*** | |
| Joining fee | VISA CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 36,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$20 |
| | |
| Membership fee | VISA CLASSIC-Tzs 72,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 150,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 210,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 72,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 150,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$100 |
| | |
| Add on fee | VISA CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 75,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 105,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 75,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$50 |
| | |
| Joining fee - Add on | NIL |
| Int. rate per month | VISA CLASSIC-3.5% |
| | VISA GOLD-3.5% |
| | VISA PLATINUM-3.5% |
| | MASTERCARD CLASSIC-3.5% |
| | MASTERCARD GOLD-3.5% |
| | MASTERCARD GOLD USD-3.5% |
| | |
| Late Payment Fee | VISA CLASSIC-Tzs 12,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 12,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 12,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 12,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 12,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$ 2 Plus 1.5% of Total Outstanding |
| | |
| Cash advance | VISA CLASSIC-3.5% of the amount or Tzs 3,600 which ever is higher |
| | VISA GOLD-3.5% of the amount or Tzs 3,600 which ever is higher |
| | VISA PLATINUM-3.5% of the amount or Tzs 3,600 which ever is higher |
| | MASTERCARD CLASSIC-3.5% of the amount or Tzs 3,600 which ever is higher |
| | MASTERCARD GOLD-3.5% of the amount or Tzs 3,600 which ever is higher |
| | MASTERCARD GOLD USD-1% of withdrawal, Min 2/- |
| | |
| Cheque bounce | VISA CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 36,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$15 |
| | |
| Over limit fee | VISA CLASSIC-2.5% of excess over credit limit or Tzs 14,000 which ever is minimum |
| | VISA GOLD-2.5% of excess over credit limit or Tzs 14,000 which ever is minimum |
| | VISA PLATINUM-2.5% of excess over credit limit or Tzs 14,000 which ever is minimum |
| | MASTERCARD CLASSIC-2.5% of excess over credit limit or Tzs 14,000 which ever is minimum |
| | MASTERCARD GOLD-2.5% of excess over credit limit or Tzs 14,000 which ever is minimum |
| | MASTERCARD GOLD USD-0.5% Of Over Limit Amount, Min 10/- |
| | |
| Chargeback fee | VISA CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 36,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$15 |
| | |
| Duplicate statement | VISA CLASSIC-Tzs 6,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 6,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 6,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 6,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 6,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$5 |
| | |
| PIN Regeneration | VISA CLASSIC-Tzs 12,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 12,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 12,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 12,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 12,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$5 |
| | |
| Card Replacement | VISA CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | VISA GOLD-Tzs 36,000 |
| | VISA PLATINUM-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD CLASSIC-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD-Tzs 36,000 |
| | MASTERCARD GOLD USD-$20 |
| | |
| Cross Currency Mark-up Fee | VISA CLASSIC-4% |
| | VISA GOLD-Tzs 4% |
| | VISA PLATINUM-4% |
| | MASTERCARD CLASSIC-4% |
| | MASTERCARD GOLD-4% |
| | MASTERCARD GOLD USD-4% |

**Cross Currency Mark up is 4% on international transactions*

## INDICATIVE FIXED DEPOSIT RATES

TZS INDICATIVE FIXED DEPOSIT RATES (% p.a.)

| Amount | 30 - less than 90 days | 90 days and < 180 days | 180 days and < 1 yr | 1 yr and < 2 yrs | 2 years and above |
|---|---|---|---|---|---|
| <100m | 1.95% | 2.85% | 3.00% | 3.85% | 7.50% |
| 100m-500m | 2.15% | 3.00% | 3.50% | 4.75% | 8.00% |
| 500m-1bn | 2.50% | 3.30% | 4.25% | 5.75% | 8.50% |
| 1bn and above | 2.75% | 3.50% | 4.75% | 6.50% | 9.00% |

USD FIXED DEPOSIT RATES (% p.a.)

| Amount | 30 - less than 90 days | 90 days and < 180 days | 180 days and < 1 yr | 1 yr and < 2 yrs | 2 years and above |
|---|---|---|---|---|---|
| <100k | 0.50% | 1.00% | 1.50% | 2.00% | 2.50% |
| 100k-500k | 0.75% | 1.50% | 1.75% | 2.50% | 3.25% |
| 500k-1m | 1.50% | 1.75% | 2.00% | 2.75% | 3.50% |
| 1m and above | 1.75% | 2.00% | 2.50% | 3.00% | 3.75% |

EUR/GBP FIXED DEPOSIT RATES (%p.a)

| Amount | 30 - less than 90 days | 90 days and < 180 days | 180 days and < 1 yr | 1 yr and < 2 yrs | 2 years and above |
|---|---|---|---|---|---|
| <100k | 0.25% | 0.50% | 0.75% | 1.00% | 1.00% |
| 100k-500k | 0.50% | 0.75% | 1.00% | 1.25% | 1.25% |
| 500k-1m | 0.75% | 1.00% | 1.25% | 1.50% | 1.50% |
| 1m and above | 1.00% | 1.25% | 1.50% | 1.75% | 1.75% |

| LOANS | |
|---|---|
| (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 2.70% |
| (i) Personal loans | 18% - 24% TZS 10$ USD |
| (ii) Overdrafts | 19% Tzs and 10% USD |
| (iii) Mortgage finance | 17% - 20% TZS 10% USD |
| (iv) Asset finance | 9%USD -19%TZS |
| (b) Unpaid loan instalment | 27%pa for local curreny and 14.5.% p.a for USD |
| (c) Early repayment | 5% pa for mortgage loan vs 5% pa for personal and vehicle loan |
| (d) Valuation fees | As per Valuer |
| (e) Other | N/A |

*Mark up is 4% on international transactions

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

The Bank was penalised Tshs 5.3 million for failure to comply with Guideline on sorting, counting, packaging cash depositing and counterfeits detection for the quarter ended 30th June 2020. We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

For more details call 080 078 0111 or visit www.eximbank.co.tz

EXIM BANK
Innovation is life

# NMB yafadhili maonyesho Nanenane kwa mil. 42.5/-

**Na Happy Severine,** SIMIYU

BENKI ya NMB imetoa Sh. 42,500,000 kwa ajili ya kudhamini maonyesho ya Nanenane ya Kanda ya Ziwa Mashariki yatakayofanyika kitaifa mkoani Simiyu.

Kati ya kiasi hicho, Sh. milioni 2.5 zimetumika kununua fulana 300 ambazo zitavaliwa na washiriki wakati wa maonyesho hayo.

Akikabidhi ufadhili huo wa hundi ya Sh. milioni 42.5 jana, Meneja wa benki hiyo Kanda ya Ziwa Magharibi, Sospeter Magesse, alisema kusaidia sekta ya kilimo ni fahari kwao kwani kupitia kilimo, benki hiyo imekuwa ikifanya biashara kubwa na kukuza pato na uchumi katika sekta ya kilimo.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu ambacho maonyesho hayo yamefanyika mkoani Simiyu, wametoa udhamini wa zaidi ya Sh. milioni 100.

**Tumefanikiwa kufungua akaunti 500,000 za wakulima na tangu Januari-hadi Juni mwaka huu tumefungua akaunti 86,000 kwa Mkoa wa Simiyu.**

"Katika kuunga mkono juhudi za Rais wetu wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli kwa miaka mitano ya awamu ya tano ya serikali yake, mchango wetu kama benki tumejenga uchumi imara kupitia kilimo na ufugaji," alisema Magesse.

Aliongeza kuwa ndani ya miaka miwili wamefanikiwa kufungua akaunti 500,000 za wakulima ambapo kwa Mkoa wa Simiyu jumla za akaunti 36,000 za wakulima wa pamba zilifunguliwa.

Aidha, alisema kuwa wako tayari kuendeleza uhusiano wenye manufaa kati yao na wakulima, wafugaji na wadau wengine wa kilimo ili watumie fursa vizuri zilizopo kwenye soko na kukuza mitaji ya biashara zao.

"Tumefanikiwa kufungua akaunti 500,000 za wakulima na tangu Januarihadi Juni mwaka huu tumefungua akaunti 86,000 kwa Mkoa wa Simiyu," alisema Maggesse.

Nae Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, kwa niaba ya mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alishukuru benki hiyo kwa namna ambavyo inajitoa kusaidia maendeleo ya wananchi hususani wakulima ambao ndio chanzo kikuu cha ukuaji wa uchumi wa nchi.

Kiswaga pia aliwataka wananchi wote wa mikoa ya Kanda ya Ziwa Mashariki ambayo inahusisha Simiyu, Mara na Shinyanga kujitokeza kwa wingi kushiriki maonyesho hayo ili kujifunza mambo mengi na kujionea teknolojia mbalimbali za kilimo zinavyofanya kazi.



Mwanasheria wa Manispaa ya Ubungo, Kissa Mbila (kulia), akimkabidhi cheti, mjasiriamali wa kuuza chakula cha mifugo, Neema Tarimo, kwa ajili ya kutambua mchango wake na kuwa balozi bora wa CRDB Malkia, wakati wa kongamano la wanawake wajasiriamali wa manispaa hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Katikati anayeshuhudia ni Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Mashariki, Badru Idd. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mzee Mkapa amwagiwa sifa

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WATUMISHI wa umma wa kada mbalimbali wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameeleza masikitiko kutokana na kifo cha Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

Wamesema kwa wakati wa uongozi wake, Mkapa alirejesha nidhamu, heshima na ari ya kazi kwa watumishi wa umma.

Hayo yalibainishwa juzi na Mtendaji wa Kata ya Chella katika Halmashauri ya Msalala, John Mahona, kwa kusema Hayati Mkapa alikuwa ni kiongozi muwazi, mkweli mwenye kusikiliza watu wote bila ya ubaguzi wa nafasi zao, na pia alikuwa mkweli na aliyeshirikiana na watu katika kutatua matatizo na changamoto zilizokuwa zikiikabili jamii.

Hayo yalibainishwa juzi na Mtendaji wa Kata ya Chella katika Halmashauri ya Msalala, John Mahona, aliyesema kuwa Hayati Mkapa alikuwa ni kiongozi mwadilifu wakati wa utumishi wake na aliyewafanya Watanzania kuithamini fedha na kujenga heshima juu ya matumizi yake.

Alisema kutokana na hali hiyo, kila mwananchi alifanikiwa kujenga na pia kuruhusu watu kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato, hali ambayo iliibua wafanyabiashara wadogo (Machinga).

Alisema sambamba na hilo, Hayati Mkapa pia alisaidia kuibua biashara za kimataifa na kukabiliana na changamoto za utandawazi uliokwenda sambamba na mfumo wa soko huria.

"Mkapa pia aliunganisha nchi ambazo zilikuwa na machafuko ya kisiasa zilizopo kusini mwa Jangwa na Sahara kama Burundi na Namibia aliposaidia usuluhishi na nchi hizo ili ziendelee kuwa na amani.

Kadhalika, alisema Hayati Mkapa alikuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya ugonjwa hatari wa Ukimwi. Pia Mkapa alijihusisha na masuala ya kusaidia jamii ikiwamo kuanzisha Taasisi ya Benjamin Mkapa Foundation ambayo ilihusika katika kutoa ushauri juu ya ugonjwa huo katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na misaada kwa sekta ya afya.

# Vijana walia kukosa ajira kupakia mchanga

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya vijana wanaojihusisha na kupakia mchanga kwenye magari katika eneo la Misugusugu Halmashauri ya Mji wa Kibaha, mkoani Pwani wamesema kama serikali haitaingilia kati wao kuendelea na kazi yao, kuna hatari ya kugeuka kuwa waporaji.

Wamesema kwa sasa hawapati kazi za kupakia mchanga kwani kazi hiyo inafanywa kwa magari ya upakiaji maarufu kama vijiko, hivyo wao wanakosa nafasi.

Wakizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki katika eneo la Misugusugu, walisema awali walikuwa wakipata Sh. 20,000 hadi 40,000 kwa siku kupitia kazi hiyo, lakini tangu utaratibu wa kutumia magari ya upakiaji uanze, wamekuwa wakitaabika kwa kukosa fedha za kuendeshea maisha yao.

Kiongozi wa wapakiaji hao, Martine Hassan, alisema utaratibu wao wa kupakia kwa mkono mchanga kwenye magari ilikuwa ni ajira yao inayowasaidia kulea familia, lakini tangu magari hayo yaanze wanakosa kazi za kufanya.

Ally Ibrahim na Rashid Omari, walisema miaka minne sasa tangu magari ya upakiaji yaanze, wamekuwa wakiiomba serikali kuingilia kati ili wapate kazi, lakini hakuna msaada waliopata hadi sasa na badala yake wameendelea kukaa bila kazi.

Naye Rashid Said, alisema, hali ya kusuasua kupata msaada kutoka kwa viongozi wao ili wapate kazi za kupakia inaweza ikasababisha baadhi ya vijana kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu vikiwamo ubakaji na uporaji ili waweze kuendesha maisha yao.

Akizungumzia kuhusiana na malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Vitendo Misugusugu, Salehe Libebile, alikiri magari ya upakiaji kufanya kazi ambazo zilikuwa zikifanywa na vijana hao.

Alisema kwa sasa anatarajia kuzungumza na wenye mashamba unapochimbwa mchanga ili waweze kuwapa kazi vijana hao.

"Wenye mashamba ya mashimo ya mchanga wameanzisha utaratibu wa kuchukua magari ya upakiaji mchanga, hivyo nitakachofanya kuwasaidia hawa vijana nitaonana na kila mwenye shamba lenye simo na kumshauri kutumia vijana wa upakiaji ili nao wapate vibarua na kuendesha maisha yao," alisema mwenyekiti huyo.

Nipashe
TESA
Jumanne Julai 28, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · S



Ukurasa 14

**Warudi likizo ni 'watupu' darasani, walimu nao waponyokwa malengo**



Ukurasa 13

Ndivyo alivyozima vibatari vijijini kwa kuwasha umeme



Ukurasa 12

**...ameondoka akiacha wazo la kuboresha elimu**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mkapa atakavyokumbukwa maendeleo ya elimu ya juu

KATIKATI ya mwaka 1990, Benjamin Mkapa anakuwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Aliingia katika nafasi hiyo akitokea Wizara ya Habari na Utangazaji.

Akiwa waziri kwenye eneo hilo, alibeba jukumu la kusimamia elimu ya vyuo vikuu, lakini pia kupanga mipango, kubuni sera, miongozo na kutunga sheria ili kuafanikisha azma hiyo.

Lakini pia bila kusahau kufanikisha matumizi ya sayansi na teknolojia nchini.

Aidha, Mkapa ndiye aliyekuwa na jukumu la kusimamia na kuwezesha wasomi na wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za umma kufanya utafiti kwa ajili ya kutatua matatizo ili kuleta maendeleo ya taifa.

Katika kusherehekea maisha ya ushindi aliyoishi Mkapa pamoja na kutafakari kifo chake wakati huu wa maombolezo, wasomi, vyuo vya elimu ya juu na wanafunzi wamuenzi kwa jitihada kubwa alizofanya za kuendeleza elimu ya juu kwa kuanzisha Sheria ya Vyuo Vikuu mwaka 2005 na pia kuunda Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Anakumbukwa kuwa katika uhai wake, alianzisha mabadiliko kwenye sekta ya elimu ya juu na kuwa kiongozi wa kitaifa aliyeasisi na kutoa nafasi kwa sekta binafsi kumiliki vyuo vya elimu ya juu na kusaidia juhudi za taifa za kusomesha Watanzania ili wafikie elimu hiyo.

Kaimu Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo), Prof. Andrew Mollel, anasema Mkapa anasifika kwa kuanzisha bodi na kuhakikisha kuwa serikali inagharamia elimu ya juu.

Anasema hilo lilileta mabadiliko ambayo pamoja na kufundisha Watanzania wengi zaidi vyuo vikuu, aliondoa ubaguzi na vikwazo ambavyo vingewakwamisha watoto wa Tanzania katika kufikia hatua hiyo.

Profesa Mollel ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Viongozi ya Vyuo Vikuu vya Binafsi, anamsifia Mkapa aliyewaandaa vijana wa Tanzania kupata elimu ya juu na kwa utaratibu ambao ni endelevu na kwamba watamkumbuka kwa kufanya uamuzi unaoongeza chachu ya maendeleo ya taifa.

Profesa Molell anasema katika uongozi wa Mkapa Sheria ya Vyuo Vikuu na mpango mzima wa maboresho ya elimu ya juu vilipatikana na kuliwezesha taifa kuwa na vyuo vikuu vingi lakini sekta binafsi hadi sasa ina idadi kubwa ya vyuo hivyo ikilinganishwa na vile vya umma.



Anaamini kuwa Rais Mkapa aliendelea kusimamia hoja ya elimu bora, elimu ya juu kwa wote waliokuwa na vigezo na pia kuipa nafasi sekta binafsi kuwa mhimili wa uchumi na wakati huo ikiwa sehemu ya wamiliki wa vyuo vikuu vya umma.

Aidha, mhadhiri mwingine, anayezungumzia mchango wa Mkapa katika elimu ya juu anasema anakumbukwa kuwa katika uhai wake alianzisha bodi iliyokuwa inatoa mikopo kwa wanafunzi wote bila kujali wanasoma vyuo vya serikali, binafsi vya kidini au ni vya kimataifa.

"Aliamua elimu ya juu kugharamiwa na serikali akiwa na imani kuwa wanaosoma ni watoto wa Watanzania. Watafanyakazi kwa ajili ya taifa lao. Hii ni heshima kubwa kwa Mkapa, Anasema Dk. Kamugisha Byabato wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustine Tanzania (SAUT).

Anasema Mkapa amebeba heshima na adhma kutoka kwa vijana waliopata mikopo, wazazi na walezi wao na kwa ujumla kazi aliyoifanya ya kuanzisha bodi inaendelea hadi sasa tena kwa mafanikio zaidi.

Dk. Byabato anasema Mkapa alikuwa na msukumo mpya katika elimu ya juu na mojawapo ya mafanikio ni kufanikisha kupatikana vyuo vikuu vinavyojitegemea badala ya kubakia kuwa mfumo wa vitivo vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kwa mfano, anasema Chuo cha Ardhi kwa miaka kadhaa kilikuwa sehemu ya UDSM. Mwaka 1996 wakati wa uongozi wa Mkapa kilikuwa chuo kikuu kishiriki, wakati akiwa madarakani mipango ikaandaliwa kukipa hadhi ya kuwa chuo kikuu na mwaka 2007 kilibadilika rasmi na kuwa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) na kuondoka kwenye kundi la vitivo au vyuo vikuu vishiriki.

Anakumbusha kuwa ARU taasisi iliyoanzishwa miaka 60 iliyopita iliwahi kufahamika kama Ardhi Institute na baadaye ikawa UCLAS lakini katika kipindi cha uongozi wa Mkapa taratibu zilianza kuandaliwa na ilipofika mwaka 2007 kilitangazwa kuwa chuo kikuu kamili.

Aidha, Chuo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), kilichopewa hadhi ya kuwa chuo kikuu mwaka 2007 na kukiwezesha kusimama chenyewe badala ya kuwa Chuo cha Elimu ya Afya cha UDSM.

MABORESHO VYUO VIKUU

Kazi ya uundwaji HESLB na utoaji wa mikopo katika vyuo vikuu ulikwenda pamoja na uboreshaji wa elimu ya juu ukilenga kuongezwa idadi kubwa ya wanafunzi vyuoni wakiwamo wanawake kusoma kozi za sayansi na uhandisi na kuweka mazingira bora ya kitaaluma vyuoni.

Baadhi ya viongozi walioshiriki kwenye uboreshaji huo ni Profesa Penninah Mlama, ambaye alikuwa mwanamama wa kwanza Mkuu wa Taalumu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Pamoja na elimu alifanya juhudi za kuimarisha na kupandisha hadhi vyuo vya ufundi na kuviwezesha kuwa vya kisasa na kiteknolojia zaidi.

Kwa mfano wakati wa uongozi wa Rais Mkapa Chuo cha Ufundi Dar es Salaam kiliboreshwa zaidi na kuwa Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam (DIT).

Katika hili Mkapa aliendelea kusimamia elimu na kuvipa sura mpya vyuo vya kati kama Dar Technical kwa kuvibadili kuwa taasisi zenye hadhi ya juu na kutoa elimu ya juu zaidi kwa mafundi mchundo (technicians).

Muendelezo huo ulifanikisha kuboresha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST).

Katika kuhakikisha kuwa elimu ya ufundi inakuwa na tija na inasimamiwa ili kuzalisha wahitimu bora, inakuwa na mitaala inayoendana na wakati kipindi cha uongozi wa Rais Mkapa, liliundwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) mwaka 1997.

ELIMU NA SABATO KASIKA

# Mkapa ameondoka akiacha wazo la kuboresha elimu



LICHA ya Rais mstaafu Benjamin Mkapa kuondoka, amewaachia Watanzania 'homework' ambayo ni wazo alilolipendekeza la kuwapo kwa mjadala wa kitaifa unaoshirikisha watu wa kada zote kujadili namna bora ya kuboresha elimu nchini.

Wazo la kiongozi huyo aliyefariki dunia wiki iliyopita, linatokana na kuwapo kwa changamoto mbalimbali kwenye sekta ya elimu ambazo zinapaswa kujadiliwa ili kupatia ufumbuzi wa kudumu.

Miongoni mwa changamoto hizo ni matokeo duni ya ujifunzaji kwa wanafunzi, utoro wa walimu na umahiri duni wa kufundisha, kukosekana kwa usawa wa kijinsia, kutojumuishwa kwa watoto wenye mahitaji maalum na mazingira magumu na ukatili uliokithiri shuleni.

Vilevile kukosekana kwa falsafa na malengo ya elimu vinavyoeleweka kwa kila mtu nalo ni tatizo, na kusababisha elimu ya Tanzania imekosa falsafa na malengo ya kuiongoza na pia ukosefu wa miundombinu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na uhaba wa majengo ya shule.

Katika jitihada za kuboresha elimu nchini, serikali imejitahidi kwa kiasi chake kupitia njia mbalimbali ukiwamo mpango wa kitaifa wa matokeo makubwa sasa, Tanzania imefanikiwa katika ujenzi wa shule za kata.

> "Naambiwa kuwa elimu yetu ndio iko chini zaidi katika nchi wanachama za jumuiya ya Afrika Mashariki, sina hakika kwa kuwa sifahamu, hata hivyo ni muhimu kuwa na mjadala wa kitaifa ambao utakuwa shirikishi bila kujali kada ya raia," anasema Mkapa.

Wazazi na walezi wamehamasishwa kuchangia madawati na ujenzi wa nyumba za walimu na mengi mengine ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya elimu nchini ili kuhakikisha walimu na wanafunzi wanatimiza wajibu wao vizuri.

Kwenye mwendeleo huo wa kuboresha elimu nchini, kuna utoaji wa elimu bure kuanzia ngazi ya shule za msingi hadi kidato cha nne, ingawa changamoto hizo bado zipo.

Hali hiyo ndiyo iliyomuibuwa rais huyo mstaafu kuja na wito huo ambao aliamini kwamba, unaweza kusaidia kusukuma mbele elimu ya Tanzania iwapo litafanyiwa kazi.

Mkapa ambaye alikuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma anasema hayo katika ya hotuba yake moja ya shughuli za chuo hicho mwanzoni mwa mwaka 2018 na kusisitiza mjadala wa kitaifa.

MJADALA KITAIFA

Katika moja ya maoni yake, Rais Mkapa aliwahi kushauri kuwapo kwa mjadala kitaifa nchini ukishirikisha watu wa kada mbalimbali ili waweze kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha elimu nchini.

Wazo lake alilitoa mwanzoni mwa mwaka juzi akionyesha kushangazwa na matokeo mabaya, ambayo yalikuwa akishuhudiwa kila mwaka kutoka kwa shule za serikali ikilinganishwa na zile za binafsi.

Katika uhai wake, anasema, umefika wakati sasa mfumo wa elimu kutazamwa upya ikiwa kwa kuangalia changamoto zinazoikabili sketa hiyo ili kubaini wapi kuna dosari, ili kuboresha elimu inayotolewa kwa shule za serikali.

"Naambiwa kuwa elimu yetu ndio iko chini zaidi katika nchi wanachama za jumuiya ya Afrika Mashariki, sina hakika kwa kuwa sifahamu, hata hivyo ni muhimu kuwa na mjadala wa kitaifa ambao utakuwa shirikishi bila kujali kada ya raia," anasema Mkapa.

Wazo lake linakuja baada ya kujiuliza ni kwa nini kila matokeo yanapotangazwa na baraza la mitihani, kati ya shule 10 zilizofanya vizuri kitaifa hazikosi shule nane za binafsi huku kukiwa na shule mbili za serikali.

Hali hiyo inamfanya ahisi kuna tatizo na kushauri kuangaliwa upya kwa mfumo wa elimu ili uendane na mahitaji ya sasa, huku akiweka wazi kwamba inawezekana baadhi ya watu wakalalamika kwa wazo hilo.

Alikuwa akikiri kuwapo kwa juhudi zilizofanywa na serikali katika kuboresha elimu, lakini suala la kuwapo kwa mjadala wa kitaifa likawa kichwani mwake kwa ajili ya kushirikisha wadau wote na watu wa kada mbalimbali.

Amefariki dunia akiamini kwamba shule za serikali zimekuwa hazifanyi vizuri, katika mitihani ya kitaifa ikilinganishwa na za binafsi ambazo mara nyingi zinaongoza katika matokeo ya mitihani ya taifa.

Hivyo ili kuboresha elimu nchini, kuwapo kwa mjadala wa kitaifa hakuepukiki, na ushauri huo unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

SHULE ZILIVYO

Baadhi ya shule za msingi na sekondari nchini, zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa miundombinu ya madarasa, hali ambayo husababisha baadhi ya wanafunzi kusomea chini ya miti.

Mazingira hayo kwa namna moja au nyingine yanaweza kuwa yanachangia kushusha kiwango cha ufaulu kwa baadhi ya wanafunzi, hivyo ushauri wa Rais Mkapa ni wa muhimu.

Ushauri unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kama vile miundombinu ya shule, kutoa vifaa vya kujifunzia kwa usawa, na kuboresha utendaji wa walimu kwa kutoa mafunzo ya ualimu kazini na motisha.

Wakati huu ambao Watanzania wanaomboleza msiba huo mkubwa, ni vyema kuzingatia kumuenzi Rais Mkapa kwa kuanzisha mjadala huo unaolenga kuboresha elimu ambalo ni wazo lililoasisiwa naye.

Hayati Mkapa alikua hajui tatizo ni nini, ni lugha, ratiba ya masomo, ushirikiano au ni ushirikishwaji wa wanafunzi, wakufunzi, wazazi au tatizo ni nini ndiyo maana anakuja na ushauri huo.

Kiongozi huyo mstaafu anaamini kwamba, mjadala wa kitaifa, unaweza kutoa jawabu la wapi sekta ya elimu haijaenda vizuri ili marekebisho yafanyike ili nchi isonge mbele kielimu.

Mkapa ametangulia lakini ameachia Tanzania wazo hilo, kwa lengo la kuboresha elimu, hivyo kazi imebaki kwa Watanzania kulifanyiwa kazi kama njia mojawapo ya kumuenzi.

Kwa kuwa moja ya dhamira kubwa ya serikali ni kutoa ni kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha udhibiti ubora na ukaguzi wa shule, kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Hatua hiyo ikichagizwa na mjadala wa kitaifa ambao ni wazo la Rais Mkapa, changamoto kwenye elimu zinaweza kupungua, hasa kutokana na ukweli kwamba unalenga kuhusisha wadau wote wa kada mbalimbali.

TEKNOLOJIA

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Mkapa alivyozima vibatari vijijini kwa kuwasha umeme



ZAMA hizi huwezi kutofautisha maisha ya mijini na vijijini kutokana na huduma nyingi zinazopatikana na kuwawezesha Watanzania kufurahia na kuishi maisha ya kisasa zaidi bila kujali eneo walipozaliwa.

Washabiki wa kandanda vijijini kama walivyo wa mijini wanapata burudani kwa kuangalia mechi za kimataifa zinazopigwa kwenye dimba za ughaibuni zikiwamo Ligi za Uingereza, Hispania na Ujerumani.

Yote hiyo ni kwa sababu vijiji karibu vyote nchini kama ilivyo miji vina umeme. Unaweza kuwa wa gridi ya taifa, umemejua au upepo na maisha yamebadilika si zama za kutumia vibatari bali ni wakati wa kuwasha umeme.

Hatua hiyo ya kubadili maisha ya Watanzania ili waondoke gizani na kuingia kwenye nishati angavu ni maono ya uongozi wa Rais mstaafu Benjamini Mkapa , ambaye baada kubaini kuwa, maji yalishapewa kipaumbele pengo lilibakia kwenye umeme.

Huenda aliamua hivyo kwa vile katika awamu za mwanzo suala la kuwafikishia wananchi maji vijijini lilikuwa kipaumbele na viongozi hao waliyataja maji kuwa ni hitaji la msingi na la muhimu kwa wanavijiji.

Katika awamu hizo serikali ililenga kuwafikishia wananchi wote maji hadi mlangoni bila kujali wanaishi mijini au vijijini.

Lakini, kwa awamu ya tatu iliyoongozwa na Rais Benjamin Mkapa, iliamini kuwa maji yanaondoa umaskini kwa kuepusha watu na maradhi na kuwahakikishia usafi, lakini iliutaja umeme kuwa ni hitaji la muhimu vijijini ili nchi iwe na maendeleo endelevu kwa kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana kutokana na kuunganishwa na umeme.

Serikali ya Mkapa ilitafsiri kwa vitendo kuwa teknolojia na nishati ni masuala yanayokwenda pamoja, kwa hiyo taifa lisingeweza kufikia maendeleo , kutumia teknolojia wala kunufaika nayo bila kila kona ya Tanzania kuwa na umeme.

Ndiyo dhana ya serikali ya awamu ya tatu kuanzisha chombo cha kusimamia usambazaji wa nishati vijijini.

Rais Mkapa anayeweza kuitwa baba wa mageuzi ya taasisi zote nchini, leo mwili wake unapoagwa Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam, baada yakufariki dunia kwa mshituko wa moyo, serikali yake ndiyo iliyosimamia kuundwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Taasisi hiyo ya serikali ambayo ilianzishwa na sheria ya mwaka 2005, ilianza kazi zake ikiwa ndani ya Wizara ya Nishati na Madini, na imefanikisha kusambaza umeme vijijini na kuwawezesha wanavijiji kuanzia Mtwara hadi Musoma, Tanga mpaka Tabora , Dar es Salaam hadi Dakawak kuachana na taa za mafuta, vibatari na kutumia umeme.

Serikali ya Mkapa ndiyo mwasisi wa Sheria ya Mabadiliko na Maboresho ya Sekta ya Nishati mwaka 2005 (Energy Sector Reform Act). Sheria hiyo ilitanguliwa na sera ya taifa ya nishati ya mwaka 2003.

Wanavijiji wanapowasha umeme leo wataendelea kumkumbuka Mkapa kuwa serikali yake ilihusika na kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund - REF) uliowezesha kuondoa vibatari majumbani.

REA ambayo ilianza kazi kuanzia mwaka 2007 miaka miwili baada ya Mkapa kuondoka Ikulu, ilikuja kutimiza maoni ya serikali kuwa umeme ni hitaji muhimu kwa kila Mtanzania na ni lazima kuwe na chombo cha kuufikisha

> Umeme umewawezesha Watanzania kunufaika na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kupitia simu ndogo na kubwa 'simu janja' ambazo zimewawezesha kuwasiliana wao kwa wao...

vijijini ambako kuna Watanzania wengi.

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya kuona kuwa zamani juhudi nyingi zilijikita kwenye kuwapa wananchi maji vijijini bila kujali kuwa umeme nao ulihitajika pia ili kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi na kuabadili maisha ya Watanzania.

REF na REA zimewezesha upatikanaji wa umeme na kuhamasisha matumizi ya nishati bora vijijini kwa maendeleo endelevu.

Hadi sasa zaidi ya asilimia 80 ya vijiji vya Tanzania vinaelezwa kuwa vina umeme. Kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati ya mwaka 2020/21 hadi Aprili mwaka huu vijiji 9,112 vilikuwa na umeme na vichache vinatarajiwa kupata nishati hiyo wakati wowote kuanzia sasa.

Kuwapo kwa umeme kila mahali nchini imekuwa fursa kwa wanavijiji kuanzisha miradi ya maendeleo kama mashine za kusaga na kusindika nafaka na kuyaongezea thamani mazao yao na kupata zaidi kuliko kama wangeyauza ghafi.

Yalikuwa maono ya serikali ya Mkapa kuwa umeme ni ufunguo kwa elimu vijijini kwani kuwapo kwa shule vijijini hasa za kata kungefanikiwa zaidi iwapo zitapata umeme.

Wanafunzi kwenye shule za sekondari za kata wameweza kujisomea wakati wote kwa vile kuna umeme. Umeme kuwaka kumewezesha kuwapo na maabara na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehema) na matumizi ya kompyuta.

Kupitia REA serikali ilikuwa na uhakika kuwa iwapo umeme utafika vijijini huduma za matibabu zinazoambatana na vipimo kwenye maabara vingepatikana kwenye zahanati za vijiji na vituo vya afya vya kata.

Katika hilo, serikali ingekuwa imefikia hatua kubwa ya kupambana na adui maradhi ambaye ni changamoto hasa kwa wakazi wa vijijini.

REA yalikuwa maono ya awamu ya Mkapa ambayo hata sasa yanaishi kwa kuwa imefikisha umeme vijijini na kufungua milango ya uwekezaji maeneo hayo na hata kuliwezesha taifa kuwekeza kwenye utalii wa kitamaduni na pia kuwahamasisha wawekezaji kufika maeneo hayo kuweka vitega uchumi.

Umeme umewawezesha Watanzania kunufaika na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kupitia simu ndogo na kubwa 'simu janja' ambazo zimewapewezesha kuwasiliana wao kwa wao pia nje na ndani ya nchi.

Lakini, pia vijijini kuna uelewa mkubwa wa masuala ya kijamii , kiuchumi , kisiasa na kiutamaduni unaoletwa na mwamko wa kufahamu habari kupitia televisheni, redio, mitandao ya kijamii, ujumbe wa simu (SMS) yote hayo yamefanikishwa na kuwapo kwa umeme.

Nishati hiyo ndiyo chachu inayowawezesha wananchi kutumia mitandao mbalimbali ya mawasiliano kama simu, kompyuta, vituo vya, redio, televisheni na intaneti, popote walipo bila kujali ni kijijini.

Wameweza kupata taarifa muhimu, burudani, kujisomea na kujielimisha popote walipo iwe mijini au vijijini. Hata wakati huu kwa kutumia simu, wanawasiliana na wagombea kwa ufanisi katika jitihada za kufanikisha uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, 2020.

Maono hayo ya REA yamewafanya Watanzania vijijini kuwa na tafsiri mpya ya maisha kulingana na jinsi wanavyotumia Tehema na kubadili mifumo ya maisha duni waliyokuwa nayo.

ELIMU

NA HAPPY SEVERINE, BARIADI

# Warudi likizo ni 'watupu' darasani, walimu nao waponyokwa malengo

- Wakiri kutogusa daftari miezi 3
- Shida? Wazazi, umaskini na mila

LIKIZO ndefu ya wanafunzi kukaa nyumbani, ilitokana na mlipuko wa homa ya mapafu Covid 19. Ndani ya Bariadi imewajia na shaka ya uwezekano kukwama malengo waliyojiwekea kitaaluma.

Huo ni wasiwasi unaotokana na wanafunzi wengi kuanzia darasa la awali hadi la tatu, walirejea shule wakiwa wamesahau vitu vingi walivyofundisha kabla.

Sasa inafika hatua inawalazimu walimu wa shule mbalimbali kurudia upya kufundisha mada zilizokwishafundishwa, kutokana na kinachojiri darasani, walichofunzwa kimesahaulika, hata walimu wanaamua kuyarudia uliowakabili wanafunzi upya darasani.




Mandhari na ofisi za shule wilayani Bariadi zilizokumbwa na mkasa wa kitaaluma, katika likizo ya corona. **PICHA ZOTE: HAPPY SEVERINE.**

**LAO WALIMU**

Pendo Manuel, ni Mwalimu katika Shule ya Msingi Mahaha, Bariadi anayesema tangu wafungue wamekuwa wakipata wakati mgumu kurudia mada zilizofundishwa, kwani wanafunzi wengi yamewatoka waliokwishafundishwa.

"Changamoto kubwa tunayokutana nayo kwa sasa, ni wanafunzi wengi wa darasa la awali mpaka la tatu wamesahau mambo mengi waliokuwa wamejifunza kabla ya kwenda likizo ya corona.

"Hivyo, tunalazimika kuanza upya kufundisha na tunapata hofu kubwa kukamilisha mipango yetu ya kuwa na ufaulu mkubwa," anafafanua Mwalimu Manuel

Anasema mkoa ulizindua mkakati wa wanafunzi kusoma wakati wa likizo ya tahadhari ya corona, mfumo ulioelekezwa zaidi katika madarasa yenye mitihani kwa shule za msingi na sekondari na kuyasahau madarasa mengine.

Manuel anasema, kwa hali hiyo walimu wengi waliweka nguvu zaidi katika wa madarasa hayo na kusahau madarasa mengine yanayohitaji msaada wa karibu wa kusoma, pindi wanapokuwa majumbani.

"Wizara na wadau mbalimbali wa elimu walijitahidi kutoa elimu kwa njia ya runinga na radio, lakini masomo na vipindi vingi vilivyokuwa vilivyokuwa vikitolewa vilikuwa vinawalenga madarasa ya juu na kuyasahau mengine," anasema Mwalimu Manuel

John Makene, ni Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Kidinda, anasema wazazi na walimu walijiwekea malengo ya kupandisha ufaulu katika shule zao, hali ambayo imekuwa tofauti baada ya uwepo wa mlipuko wa homa ya mapafu.

"Sio siri, sisi walimu tunahofu kubwa sana kama malengo yetu tuliyokuwa tumejiwekea kama yataweza kufanikiwa, kwani likizo ya corona imewafanya wanafunzi wengi kushuka viwango vyao vya uelewa," anasema Mwalimu Makene.

Anaeleza uzoefu katika kipindi cha likizo ya corona, wazazi wengi waliwatumia watoto wao kama kitega uchumi kwa kuwapa kazi nyingi za nyumbani, biashara ndogo mitaani na vibarua mashambani, huku wanashindwa kuwapatia muda wa kusomea na kufanya mazoezi ya masomo.

Rajab Madaraka, ni mwalimu katika Shule ya Msingi Gamondo, wilayani hapa, anasema unahitajika muda na nguvu za ziada kwa shule ziweze kufikia malengo waliojiwekea awali katika kupandisha ufaulu wa shule zao.

**WAFANYEJE WALIMU?**

Madaraka anasema idadi kubwa ya wanafunzi wamerudi kama wanaanza upya na hasa kwa wale wa madarasa ya awali hadi la tatu na wengi wao wamerudi hawana madaftari yao huku wakieleza kutokujua yalipo.

Geofrey Kamugisha, ni Mwalimu wa Taaluma katika Shule ya Msingi Kidinda, anasema kuwa katika nafasi yao ya ualimu, wameshakutana kujadilia namna ya kukabili upungufu uliojitokeza.

Mwalimu Kamugisha katika nafasi yao ya ualimu, wamejipanga kuhakikisha wanafundisha staili ya kasi na kuongeza muda, kukidhi kuziba pengo linalotakiwa.

Anasema katika wakati wa likizo, waligawana majukumu na mazoezi kwa madarasa ya mitihani, lakini kwa bahati mbaya waliyasahau madarasa mengine na ndio maana wanakuwa na hofu kubwa ya kuyafikia malengo yetu.

**WAZAZI WAO**

Baadhi ya wazazi katika vijiji vinavyozunguka jamii jirani, wanasema kuwa desturi na mila zao suala la kuwafanyisha kazi watoto mashambani, kuchunga mifugo na biashara ni sehemu ya maisha.

Wanasema kuna mazoea jamii kutoelekeza kipaumbele kwa elimu, kama ilivyo kwa mikoa mingine na ndio sababu inayowafanya kutothamini elimu kwa watoto, hali inayowakwaza kujifunza na kujisomea katika elimu yao ya msingi shuleni.

Amosi Maunga, ni mkazi wa Kidinda mjini Bariadi, anasema wakati wa likizo itokanayo na tahadhari ya corona, wanafunzi wengi wa shule za msingi na sekondari walizagaa mitaani katika biashara, kufaya kazi shambani na watoto wanakosa muda wa kujisomea.

"Historia ya mazingira ya wakazi na wazaliwa wa Bariadi, hawajawahi kuipa elimu kipaumbele na ndio maana wakati wa likizo hiyo, hawakuweza kuwasaidia watoto wao," anatamka Masunga.

"Waliwaacha bila ya kusoma na ndio maana wengi wamesahau hata masomo waliyokuwa amefundishwa," anaeleza, huku mwenzake Mwalimu Peter Luhumbila, analifafana kuwa:

"Ni aibu kubwa sana kwa kusikia eti wanafunzi wa madarasa yasiyo ya mitihani, eti wamesahau walichofundishwa na walimu kurudia upya.

"Hii inadhihirisha wazazi hawakutimiza wajibu wao pindi watoto wao wakiwa katika likizo ya tahadhari ya corona,"

**WANAFUNZI**

Kuna baadhi ya wanafunzi wa madarasa ya chini walitumia likizo hiyi iliyopita kujishughulisha na kazi za nyumbani kama kuvuna mpunga na wengine katika biashara ndogoo walizokuwa wakielekezwa na wazazi wao.

Baraka Guga, yuko darasa la tatu katika Shule ya msingi Mahaha, anasema kipindi vha likizoni, alikuwa akimsaidia mzazi wake kufanya kazi za shambani na biashara ya karanga.

"Sikuwahi kusoma wakati wa likizo, hivyo vitu vingi nimevisahau na muda mwingi nilikuwa nikimsaidia mama kuvuna mpunga na wakati mwingine nilikuwa naenda kuuza karanga ili mama apate hela ya matumizi ya nyumbani," Guga

Ritha Elias, anasoma darasa la sita katika shule ya Gamondo, anasema hakuweza kupata muda wa kutosha kujisomea, kutokana na mzazi wake kumpa kazi zaidi majukumu ya nyumbani. Elias, anawashauri walimu kwa kushirikiana na serikali, ione namna ya kuwasaidia, kuwa na mifumo ya jaribio la kitaaluma, likizo kama ilivyo kwa darasa la mitihani.







# Waonywa utambuzi wa kaya

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

VIONGOZI wa serikali za mitaa na wajumbe wa nyumba 10 wametakiwa kuwa waaminifu na waadilifu katika uhakiki wa walengwa wa mpango kunusuru kaya maskini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omari Mkulo, alipokuwa akizungumza na waandishi ofisini kwake juu ya uhakiki kupitia mpango huo unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Dk. Mkulo aliwataka viongozi hao kuwa waaminifu na waadilifu katika kuzitambua kaya maskini nchini.

"Hawa viongozi ni watu muhimu kwenye kazi hii itakayoanza ya kuzitambua kaya maskini zitakazopata ruzuku ya serikali. Wao wanawajua kila mtu kwenye maeneo yao kuanzia kipato hadi familia zao zote, hivyo wasipokuwa waadilifu wataharibu nia jema ya serikali," alisema.

Alisema kazi hiyo inatarajiwa kuanza Agosti Mosi katika wilaya hiyo na wanatarajia kutoa mafunzo kwa wasimamizi kabla ya kuwapeleka kazini.

Alibainisha kuwa wasimamizi hao watakaopatiwa mafunzo idadi yao itakuwa 64, na watatawanywa kuendesha zoezi hilo katika vijiji 43 vya wilaya hiyo.

Kadhalika alisema katika mafunzo hayo watajengewa uwezo wa kushirikiana na viongozi wa maeneo husika ili kuwabaini walengwa wa mpango huo.

Dk. Mkulo alisema wasimamizi hao wataapishwa na kama watakiuka maagizo na vigezo walivyopewa watawajibishwa kutokana na uzembe huo.

Pia alisema zoezi hilo kuwatambua wahusika wa kaya maskini kwa wilaya hiyo litafanyika kwa muda wa siku tatu kutokana na nguvu kazi iliyopewa majukumu hayo.

Aidha, alisema serikali ilisimamisha kutoa ruzuku hiyo kwa lengo la awali kutokana na kubainika kwa wasio na sifa za kupokea msaada huo ambao ulikuwa na lengo la kuzinusuru kaya maskini nchini.

# Viongozi wa dini waeleza namna kumuenzi Mkapa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa madhehebu ya dini mkoani Dodoma, wameishauri serikali na Watanzania kwa ujumla kuyaenzi maisha mema, aliyoishi Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, kwa kutekeleza mambo mazuri aliyoyaasisi.

Pia wamesisitiza kuwa namna bora ya kumuenzi Rais Mkapa, ni kwa Watanzania na viongozi wote kutekeleza kwa vitendo mambo aliyoyafanya.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema Mkapa ameacha funzo kubwa juu ya namna kiongozi wa umma anatakiwa kuishi na kutenda kazi zake kwa uadilifu, haki, usawa, uwazi na ukweli.

Pia walitoa rai kwa Watanzania wote kusoma kitabu alichoandika Mkapa kitwacho 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Malengo Yangu) kwa kuwa kimejaa nasaha juu ya hekima, busara na maadili ya uongozi wa uma na utu wema kwa ujumla.

Askofu Mstaafu wa Kanisa la EAGT-Ipagala, Dodoma, Evance Chande, alisema kifo cha Mkapa kichukuliwe na Watanzania kama nafasi nzuri ya kujikagua na kujifunza namna bora ya kuishi kwa wema na kutekeleza majukumu yake kwa uwazi na haki.

**Urithi mkubwa aliyotuachia Mzee Mkapa umo katika kitabu chake ambacho kinaelezea maisha yake kwa ujumla, alivyotumia muda wake kuwatumikia Watanzania na Waafrika kwa ujumla bila kujali itikadi za kisiasa wala dini.**

"Urithi mkubwa aliyotuachia Mzee Mkapa umo katika kitabu chake ambacho kinaelezea maisha yake kwa ujumla, alivyotumia muda wake kuwatumikia Watanzania na Waafrika kwa ujumla bila kujali itikadi za kisiasa wala dini," alisema.

Pia alisema Mkapa alikuwa mstari wa mbele kuwashawishi viongozi wenzake kujenga utamaduni wa kuandika vitabu juu ya maisha yao ili kufundisha vizazi vijavyo juu ya maadili mema ya utu na uongozi wa umma.

Naye Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, aliwaomba Watanzania kuendeleza na kuishi mema aliyoyafanya Mkapa, katika kipindi chote cha uongozi wake.

"Mema aliyoyafanya ni pamoja na usimamizi bora wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara na uwanja wa mpira," alisema.

Kuhusu kusaidia taasisi za kiimani, alisema anamkumbuka Mkapa kwa jitihada kubwa alizofanya katika kukamilisha ujenzi wa msikiti mkubwa wa Gaddafi ulioko Dodoma.

Walisema kuwa mazuri ambayo Mkapa alikuwa akiyatenda ni pamoja na kutetea haki, usawa na amani, ili ukuaji chanya wa jamii na uchumi nchini Tanzania na bara zima la Afrika.

Aidha, walizungumza pia Mkapa alivyotumia vema muda wake baada ya kustaafu katika kutetea amani barani Afrika kwa kutumia elimu, hekima na uzoefu wake kutatua migogoro mbalimbali iliyokuwa inazikabili nchi mbalimbali barani Afrika na kusema huo ulikuwa mfano mzuri unaotakiwa kuigwa na viongozi aliyowaacha.

Kupitia kauli mbiu ya 'Mtaji wa Maskini ni Nguvu zake Mwenyewe' wakati wa uongozi wake, Mkapa aliamini kuwa maendeleo ya nchi yanatokana na kila mwananchi kutumia vyema nguvu, uwezo na akili yake kufanya kazi kwa bidii na kwa kumtanguliza haki.

Pamoja na mengi aliyofanya, Mkapa atakumbukwa kwa jiihada zake za kupambana na rushwa, ubadhirifu na kuwa mstari wa mbele kuchochea kukua kwa uchumi wa Tanzania.



Baadhi ya wachuuzi wa mboga, wakiendelea na biashara zao kando ya barabara nje ya soko kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, huku magari na pikipiki zikipita karibu kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Magereza yaongeza uwezo vifaa ujenzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini limenunua vifaa vya ujenzi ambavyo vitasaidia katika shughuli mbalimbali za ujenzi katika zabuni inazopata.

Mkuu wa Jeshi hilo, Kamishna Jenerali Suleiman Mzee, alisema jana kuwa vifaa hivyo vitasaidia pia kuliingizia mapato jeshi kupitia kazi mbalimbali wanazopata huku akisema huo ni mwendelezo wa kuboresha utendaji wa kazi.

Akizungumza, katika hafla ya kukabidhi greda katika Gereza la Msalato, Jenerali Mzee alisema kifaa hicho chenye thamani ya Sh. milioni 220, kimefanya idadi ya vifaa vya ujenzi katika Jeshi la Magereza kuongezeka.

Alisema anaamini hivi sasa kazi zitakwenda kwa wakati kwa kuwa kila kifaa cha ujenzi kinaendelea kununuliwa ili kuboresha kitengo hicho ndani ya Magereza.

Mbali na kifaa hicho, alisema walishanunua magari makubwa ya ujenzi matano na aina ya 'excavator' moja ambavyo vinafanya kazi ya ujenzi.

Alisema lengo ni kuona jeshi hilo halicheleweshi kazi za ujenzi ambazo wanapata kutoka katika maeneo tofauti jijini hapa na sehemu nyingine za nje ya Dodoma na kusisitiza kuwa wahusika wa kitengo hicho wanapaswa kuchangamka ili kufanya kazi kwa bidii.

Naye Mkuu wa Gereza la Msalato, Mrakibu Hamisi Nyalusi, alisema wanashukuru kupata vifaa hivyo ni muda mwafaka kwao kuchapa kazi kwa bidii ili kuhakikisha wanafanya kazi zao kiufasaha ili kuwavutia wanahitaji huduma za magereza.

Alisema lengo lao ni kuona kazi zao zinakwenda kwa ufasaha na kuongeza kuwa watafanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha wanafanikisha kile walichokabidhiwa.

Nyalusi alisema katika eneo lake kuna mchanga hivyo itakuwa kazi rahisi kufanya kazi za ujenzi za kuimarisha jeshi hilo katika miradi ya ujenzi wanayofanya na kwamba watachapa kazi kwa bidii ili kulipatia sifa jeshi kupitia kazi wanazofanya.





# Wajawazito Momba walalamikia faini kisa kujifungulia nyumbani

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

WAJAWAZITO Katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe, wamelalamikia kutozwa fedha na wahudumu wa afya kama adhabu, baada ya kujifungulia nyumbani wakidai sio makusudi kufanya hivyo bali ni tatizo la barabara na umbali wa kufuata huduma za matibabu.

Mmoja wa kinamama kutoka Kata ya Mbuyuni, ambaye alijifungulia nyumbani, Huruma Mpeta (17), alisema wanatozwa Sh. 30,000 pamoja na kunyang'anywa kadi.

Mpeta alisema baada ya kujifungulia nyumbani, alikwenda hospitalini na kuambiwa hawezi kuhudumiwa hadi apeleke hela Sh. 30,000 ndipo apate huduma za matibabu.

**Wale wote waliohusika na vitendo vya kuwatoza faini wajawazito waliojifungulia nyumbani, atawatafuta kwa ajili ya kuwachukulia hatua za kinidhamu.**

"Nilijifungulia nyumbani kutokana na matatizo ya kifamilia ikiwamo ukata wa fedha, pia umbali lakini kituo cha afya kilichoko jirani kinatutoza faini kama faini ya kutojifungulia hospitali... suala hili linatuumiza sana, tunaomba serikali iliangalia suala hili," alisema Mpeta.

Kwa upande wake, Agripina Namwichi ambaye ni mkunga kutoka Kata ya Mbuyuni, alisema mara kadhaa huwahudumia wajawazito wanaofika hapo.

Alidai baadhi ya wanaofika hapo hudai ujauzito wao umeghubikwa na mambo ya kishirikina, hivyo huenda huko kwa ajili ya kusaidiwa.

Mbali na kwamba huwazalisha kinamama, lakini hutoa ushauri wa kitaalamu ambao ni umuhimu wa kujifungulia kwenye vituo vya afya.

Mganga Mkuu Mkoa wa Songwe, Dk. Hamad Nyembea, alisema hairuhusiwi mjamzito kutozwa fedha hata kama atajifungulia nyumbani.

Alisema wale wote waliohusika na vitendo vya kuwatoza faini wajawazito waliojifungulia nyumbani, atawatafuta kwa ajili ya kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Aliwaambia wahudumu wa afya kuacha tamaa za fedha badala yake waendelee kutoa huduma bure za afya sambamba na kuwahamasisha kuhudhuria kliniki na umuhimu wa kujifungulia kwenye vituo vya afya.

Imeelezwa kuwa baadhi ya zahanati na vituo vya afya mkoani Songwe zimelalamikiwa kutoza fedha kwa wanawake wanaojifungulia nyumbani ikiwa ni kampeni ya kuhimiza wajawazito kujifungulia katika zahanati badala ya majumbani.



Baadhi ya wagombea udiwani wa viti maalum, Jimbo la Mbeya Mjini, wakiwasikiliza wagombea wenzao (hawapo pichani), wakati wakijinadi katika uchaguzi wa kura za maoni ili kuwapata wagombea 14 wa nafasi hizo kati ya wagombea 93 wanaoshiriki, jijini humo, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watoto wenye VVU wasaidiwa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

TAASISI isiyo ya Kiserikali ya HJFMRI kupitia Mradi wa Walter Reed Program Tanzania, imekabidhi msaada wa majokofu matano kwa wilaya zote za Mkoa wa Songwe.

Imesema kuwa lengo la msaada huo ni kuhifadhi dawa za watoto wenye uzito wa chini ya kilo sita wanaoishi na maambukizi ya virusi vya ukimwi (VVU).

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo kwa niaba ya Walter Reed, Dk. David Maganga alisema taasisi yake imetoa majokofu 24 ambayo yatawasaidia pia kwa mikoa ya Mbeya, Katavi na Rukwa.

Alisema watoto walikuwa wakipata usumbufu mkubwa kutokana na dawa hizo kuharibika kwa sababu ya ukosefu wa majokofu na kuwafanya watoto kuhatarisha afya zao.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Seif Shekalaghe, alisema HJFMRI imekuwa sehemu ya kutatua matatizo yanayoikabili mkoa huo.

Alisema misaada mbalimbali ya hali na mali kupitia sekta ya afya imechangia kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, zaidi katika kukabiliana na maambukizi ya virusi vya ukimwi pamoja na matumizi ya dawa za kulevya.

"Nawashukuru Walter Reed kuwa sambamba na serikali katika kuwahudumia wananchi kwa kuhakikisha mnaboresha huduma za afya ikiwa ni pamoja na kuwapatia vifaa tiba na kufanya utafiti wa magonjwa mbalimbali," alisema Dk. Shekalaghe.

Dk. Shekalaghe alisema majokofu hayo yatasaidia kuhifadhi dawa kwa uangalifu mkubwa, huku akiwasihi watumishi wa afya kuyatunza ili yaendelee kutumika kwa ajili ya kuhifadhi dawa kwa ajili ya watoto.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Hamad Nyembea, alisema msaada huo umekuja kwa wakati katika kuyafikia malengo ya Mkoa na Taifa kutoka 90 tatu.

Alisema Walter Reed imekuwa ikitoa misaada ya elimu, vifaa, dawa na raslimali watu kwa miaka 15 nchini katika mapambano dhidi ya ukimwi na dawa za kulevya, na kwamba sasa inaendelea na kujenga vituo vya tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya.

# Wanafunzi 160 wasomea chumba kimoja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya wanafunzi 160 wa Shule ya Msingi Mwasanga iliyopo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wanalazimika kukaa chumba kimoja kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa unaoikabili shule hiyo.

Hayo yalisemwa juzi na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Keneth Amon, wakati akizungumza na Nipashe ambapo alisema hali hiyo inasababisha changamoto katika ufundishaji.

Mwalimu Amon alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 1,311, lakini ina vyumba vya madarasa nane pekee na hivyo kuwa na upungufu unaosababisha wanafunzi kusongamana kwenye vyumba hivyo vichache.

Alisema ili kutosheleza mahitaji ya vyumba vya madarasa kwa idadi hiyo ya wanafunzi, vinahitajika vyumba vya madarasa 30, hivyo upungufu uliopo ni vyumba 22.

"Pamoja na upungufu huu, lakini hata hivi vyumba vilivyopo vinane vina hali mbaya sana, vimechakaa kiasi cha kuhatarisha maisha ya wanafunzi hivyo tunaomba tusaidiwe kuboresha mazingira haya," alisema Mwalimu Amon.

Pia alisema kuwa shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa madawati 140 kwa ajili ya wanafunzi na kwamba wadau wa elimu ikiwamo Benki ya NMB imekuwa ikiwasaidia vitu mbalimbali yakiwamo madawati.

Katika kukabiliana na tatizo la vyumba vya madarasa pamoja na madawati, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema ofisi yake ilipeleka maombi ya kusaidiwa kutoka kwa wadau na taasisi mbalimbali.

Alisema benki ya NMB, imekuwa ya kwanza kutoa misaada na kwamba ana matumaini wadau wengine walioombwa wataendelea kujitolea.

Alisema katika jiji hilo Benki ya NMB ilitoa msaada wa zaidi ya shilingi milioni tisa yakiwamo madawati, mabati kwa ajili ya kuezekea vyumba vya madarasa pamoja na huduma zingine muhimu ikiwamo afya.

Aliwataka wazazi na walezi wa wanafunzi kujitolea katika kuboresha miundombinu ya shule ili watoto wao wasome katika mazingira ambayo ni rafiki.

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Stratan Chilongola, alisema msaada huo ni sehemu ya utaratibu wa benki hiyo kurudisha faida kwa jamii inayowazunguka.

Alisema wanafanya hivyo kutokana na kwamba faida wanayoipata inatokana na jamii, ambayo ndiyo wateja wakuu wa benki hiyo kwa kutumia huduma za kibenki.



# TBS, ZBS zasaini makubaliano kuondoa vikwazo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), zimesaini hati ya makubaliano ya kuondoa vikwazo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika juzi katika Ofisi za Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, Waziri wa wizara hiyo, Balozi Amina Salum Ali, alisema makubaliano hayo yatarahisisha biashara na utendaji wake.

Alisema, zipo changamoto zinazojitokeza kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kuhoji biashara zao kwenda Tanzania bara na kujitokeza changamoto mbalimbali ikiwamo kusajili biashara jambo ambalo tayari limeshaanza kufanyiwa kazi.

Balozi Amina alisema, pia makubaliano hayo yatakuwa ufunguo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kuendesha biashara zao kwa urahisi na kukua zaidi.

Alisema bado vyombo hivyo vina tofauti kutokana na ZBS kuwa wachanga na kuiomba TBS kushirikiana na tasisi hiyo katika mafunzo mbalimbali ambayo yatawawezesha kufikia walipo.

Alisema changamoto ya Tanzania bidhaa bado hazijaweza kupata somo la ithibati katika biashara hivyo ni vyema TBS kuisaidia ZBS kuleta vyombo hivyo ili viweze kusaidia katika majukumu ya kazi zao za kila siku.

Hata hivyo, alisema serikali tayari imeshatoa sera ya viwanda na ushirikiano baina ya tasisi binafsi hasa katika kuwasaidia wajasiriamali wadogo ili wakue kibiashara.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Yussuf Abdalla, aliahidi ushirikiano huo unakua na kuhakikisha biashara zinakwenda vizuri bila changamoto ya kibiashara.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ZBS Zanzibar, Rahima Ali Bakar, alisema ushirikiano huo utasaidia kuwarahisishia ushirikiano wa kibiashara haina yao na Tanzania Bara na kuwataka wafanyabiashara wote kufuata sheria zilizowekwa na taasisi hizo ikiwamo vigezo vyote vya kibiashara.

# Viongozi wamkumbuka Mkapa kwa kuheshimu vyama vingi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa vyama vya siasa Zanzibar, wamesema watamkumbuka na kumuenzi Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano, Benjamin Mkapa, kwa sababu aliheshimu mfumo wa vyama vingi na kuweka misingi imara na kuiweka Tanzania katika utulivu wa kisiasa wakati wa uongozi wake.

Akizungummza na Nipashe, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ada Tadea, Juma Ali Khatib, alisema Mkapa atakumbukwa kuwa ni rais wa kwanza aliyeongoza Tanzania katika mfumo wa vyama vingi mwaka 1995 na kuweka misingi imara yenye kuzingatia usawa na demokrasia.

Alisema mfumo wa vyama vingi umepata mafanikio makubwa kutokana na uwezo wa rais mstaafu Mkapa ambaye ndiye aliyetandaza misingi mizuri ya kidemokrasia ambayo imesaidia nchi kufanya uchaguzi huru usiokuwa na vurugu wala malalamiko.

Alisema Mkapa alifanikiwa kuzishawishi nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na hatimaye kuzaliwa upya kwa jumuiya hiyo katika mwaka 1999 baada ya kuvunjika mwaka 1977.

**Katika kipindi cha uongozi wa Rais mstaafu Mkapa hakuna mtu aliyejaribu kuyachezea mapinduzi ya mwaka 1964 pamoja na Muungano wake... Mkapa alikuwa muumini nambari moja ya tunu za kitaifa.**

"Hatutamsahau Rais mstaafu Benjamin Mkapa...alikuwa kiongozi aliyefanikiwa kujenga misingi imara ya demokrasia ya siasa za vyama vingi katika mwaka 1995 ambapo pia tunamkumbuka ndiye aliyefanikiwa kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1999," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Sadalla, alisema chama hicho daima kitamkumbuka kwa kukijengea ujasiri mkubwa wa kuwa chama tawala kilichoshika dola.

Alisema ujasiri huo uliwajengea ari kubwa wanachama wa chama hicho na kufanikiwa kuchochea ushindi wake katika chaguzi mbalimbali ikiwamo uchaguzi mkuu.

"Chama cha Mapinduzi kimepata pigo kubwa kufuatia kifo cha rais mstaafu Benjamin Mkapa...aliwajengea ari na moyo wanachama kujiamini kwa sababu chama chao kimeshika hatamu na kuongoza dola," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mberwa, alisema wananchi wa kisiwa hicho hawatamsahau marehemu Mkapa kwa juhudi zake za kuleta maelewano baada ya kutokea kwa mpasuko wa kisiasa uliosababishwa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2000.

"Maridhiano ya kisiasa ya wananchi wa kisiwa cha Pemba yaliyofanywa na rais mstaafu Mkapa kwa kiasi kikubwa yalisaidia kurudi kwa amani na utulivu kwa wananchi wa Pemba na wale waliokimbia kisiwa hicho kwenda Shimoni Mombasa kurudi," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha AAFP, Said Soud, aliwataka Watanzania kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu wakati taifa likiomboleza kifo cha Mkapa.

Alimsifu Mkapa kwa ushujaa wake wa kuyalinda Mapinduzi ya Zanzibar na kuwa tayari kupambana na mtu yeyote aliyekuwa akijaribu kuuchezea ikiwamo na Muungano.

"Katika kipindi cha uongozi wa Rais mstaafu Mkapa hakuna mtu aliyejaribu kuyachezea mapinduzi ya mwaka 1964 pamoja na Muungano wake... Mkapa alikuwa muumini nambari moja ya tunu za kitaifa," alisema.




Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Modline Castiko, akifungua mkutano wa wadau kuhusu kupinga usafirishaji haramu wa binadamu Mjini Zanzibar, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TAMWA yaonya wazazi/walezi kuadhibu watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimewataka wazazi na walezi wachukue tahadhari kwa malezi ya watoto wao na waache kutumia adhabu nzito wanapofanya makosa.

TAMWA ilisema hayo kufuatia tukio la udhalilishaji lililotokea hivi karibuni Visiwani Zanzibar kwa mtoto wa miaka 14 aliyevuliwa nguo zote na mama yake wa kambo na kumtoa nje hadharani.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Mzuri Issa, alisema chama hicho kinasikitishwa na tukio hilo ambalo ni la kikatili na kawataka wazazi kutoa adhabu inayostahiki.

Alisema TAMWA ilipata taarifa Julai 21, mwaka huu kuwa mama wa kambo (jina linahifadhiwa), kumvua nguo mtoto wake kutokana na kitendo alichokifanya mtoto huyo kuingia chumbani kwa mama huyo na kuchukua mafuta ya kujipaka bila ya ridhaa yake.

"Hata kama mtoto amefanya kosa, lakini wazazi watambue kuwa hawastahiki kuwapa adhabu kali ambazo ni kinyume na haki za binadamu," alisema Dk. Mzuri.

Aliwataka wazazi kushughulikia kwa uangalifu mabadiliko ya tabia ya watoto katika hatua ya mpito ya utoto kuelekea ujana ili kuwaongoza na kuepuka mzozo usio wa lazima.

Alivitaka vyombo vya sheria kulipa uzito suala hilo kwa kutoa adhabu inayofaa kwa mhusika wa tukio hilo kwa kuwa tukio hilo limesharipotiwa katika vyombo hivyo.

# International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2020 | ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2020 |
|---|---|---|---|
| A. | *MALI* | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,691 | 1,593 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 7,346 | 6,306 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 14,096 | 9,563 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 7,787 | 3,851 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 1,174 | 804 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 43,503 | 47,375 |
| 12 | Mali Nyingine | 5,360 | 2,434 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 503 | 536 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **82,460** | **72,463** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 2,934 | 14,024 |
| 18 | Amana za Wateja | 56,951 | 37,329 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 207 | 216 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 5 | 35 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,277 | 942 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 61.22 | 60.80 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,021 | 211 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | ***JUMLA YA DHIMA*** | **63,455** | **52,818** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **19,005** | **19,645** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,025 | 20,025 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 4,408 | 4,561 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (4,377) | (4,961) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,051) | 20 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **19,005** | **19,645** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 2,357 | 1,948 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 12,187 | 12,736 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,888 | 1,256 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 23% | 27% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 23% | 26% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 89% | 94% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65% | 67% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79% | 84% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 17% | -4% |
| (vii | Ongezeko la Mali | 14% | -5% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.06.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA LINGANISHI ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2020 | 30.06.2019 | 30.06.2020 | 30.06.2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,475 | 1,860 | 3,214 | 3,558 |
| 2 | Gharama za Riba | 804 | 814 | 1,501 | 1,654 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***671*** | ***1,046*** | ***1,713*** | ***1,904*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 632 | 60 | 661 | 60 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **250** | **302** | **646** | **502** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 20 | 72 | 83 | (7) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 48 | 39 | 98 | 97 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 182 | 192 | 466 | 412 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,360** | **1,548** | **2,749** | **3,055** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 564 | 551 | 1,181 | 1,188 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 49 | 66 | 66 | 133 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 746 | 930 | 1,502 | 1,734 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,071)** | **(259)** | **(1,051)** | **(709)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | 30 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,071)** | **(259)** | **(1,051)** | **(739)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,071)** | **(259)** | **(1,051)** | **(739)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 60 | 65 | 60 | 65 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (53) | (13) | (52) | (37) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (53) | (13) | (52) | (37) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -5.54% | -0.92% | -2.72% | -1.28% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -22.23% | -5.08% | -10.90% | -7.26% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 78.83% | 71.57% | 71.21% | 75.24% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 6.11% | 5.76% | 8.45% | 5.25% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 30.06.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2020 | 30.06.2019 | 30.06.2020 | 30.06.2019 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,071) | 20 | (1,051) | (259) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 694 | 89 | 783 | 241 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,240 | 3,500 | 6,740 | 1,336 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 8,522 | (2,401) | 6,121 | 1,148 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 2,114 | (1,073) | 1,042 | (13) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,925) | 559 | (2,367) | (541) |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | -SMR | (86) | 12 | (74) | 653 |
| | - Mengineyo | 431 | 915 | 1,346 | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***10,920*** | ***1,622*** | ***12,541*** | ***2,565*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (29) | (24) | (53) | (40) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (12,516) | 4,656 | (7,861) | (7,737) |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(12,546)** | **4,632** | **(7,914)** | **(7,777)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | - | - | - | - |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(1,626)** | **6,253** | **4,627** | **(5,212)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 16,677 | 10,424 | 10,424 | 38,218 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **15,051** | **16,677** | **15,051** | **33,006** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Saini:

| | | |
|---|---|---|
| **VILLY VELLAYAPPAN** | **GEORGE MSAMBAZI** | **JOHN MWAKASONDA** |
| Ofisa Mtendaji Mkuu | Mkuu wa Fedha | Mkaguzi Mkuu wa Ndani |
| Tarehe: 22 Julai 2020 | Tarehe: 22 Julai 2020 | Tarehe: 22 Julai 2020 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

Saini:

| | |
|---|---|
| **ALFRED MKOMBO** | **CHARLES RWECHUNGURA** |
| Mjumbe wa Bodi | Mjumbe wa Bodi |
| Tarehe: 22 Julai 2020 | Tarehe: 22 Julai 2020 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2020

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020 | 20,025 | - | (4,086) | 4,140 | - | - | 20,079 |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (23) | | | | (23) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (1,051) | | | | (1,051) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (268) | 268 | | | (0.0) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Salio la mwisho wa kipindi 30.06.2020 | 20,025 | - | (4,354) | 4,408 | - | - | 19,005 |
| | | | | | | | |
| Mwaka Uliopita | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019 | 20,025 | - | (1,825) | 2,445 | 396 | - | 21,041 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (739) | | | | (739) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | - |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (99) | 122 | (23) | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Salio la mwisho wa kipindi 30.06.2019 | 20,025 | - | (2,564) | 3,132 | 464 | 9 | 20,302 |

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yafunga ubalozi wake China

**CHENGDU,** China

MAREKANI imelazimika kuufunga ubalozi wake mdogo uliopo mjini Chengdu China.

Ubalozi mdogo wa Chengdu - ulianzishwa mwaka 1985 na uliwakilisha maslahi ya Marekani katika eneo kubwa la Kusini-Magharibi mwa China, likiwamo jimbo linalo jitawala la Tibet, ambako kumekuwa na shinikizo la muda mrefu la kutaka uhuru wake.

Wengi wa wanadiploamasia zaidi ya 200 ni wafanyakazi walioajiriwa ambao ni raia wa China.

Jimbo la Chengdu linaangaliwa na Marekani kama eneo linalotoa fursa kwa mauzo ya nje ya bidhaa za kilimo, magari na mashine.

Baada ya kufungwa kwa ubalozi huo, Marekani itakuwa na balozi ndogo nne ndani ya China na ubalozi mkuu katika mji mkuu Beijing. Pia ina ubalozi mdogo Hong Kong, ambalo ni koloni la zamani la Uingereza. China ilipoteza ubalozi wake mdogo wa Houston wiki iliyopita, lakini bado ina balozi ndogo nne nchini Marekani na ubalozi wake mkuu uliopo katika mji mkuu wa Marekani Washington DC.

Jana, siku ambayo ilitajwa kuwa ya mwisho kwa wafanyakazi wa ubalozi huo walionekana wakibeba maboksi ya makablasha yao na mifuko ya takataka.

Wakati huo huo, umati wa wakazi wa eneo hilo ulikusanyika nje ya ubalozi huo, ukiwa umebeba bendera za China na kupiga picha.

China ilichukua hatua ya kufunga ubalozi huo kujibu hatua ya Marekani kuufunga ubalozi wake mdogo wa Houston, Texas, wiki iliyopita.

Baada ya muda wa mwisho uliowekwa wa saa 72 kwa wanadiplomasia wa China kuwa wameondoka Houston kumalizika Ijumaa, taarifa zinasema maofisa wa Marekani walifungua kwa nguvu mlango ili kuingia ndani ya ubalozi huo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisema kuwa serikali ya Marekani mjini Washington iliamua kuchukua hatua hiyo kwa sababu Beijing ilikua inaiba akili miliki.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Wang Wenbin, alijibu akisema hatua ya Marekani ni mkanganyiko wa uongo wa chuki dhidi ya China.

Hali ya wasiwasi imekua ikiongezeka kati ya nchi hizo mbili zenye nguvu za nyuklia juu ya masuala mbalimbali. **BBC**

## Ujerumani yapinga Urusi kurudishwa G7

**BERLIN,** Ujerumani

UJERUMANI imekataa ombi lililowasilishwa na Rais wa Marekani, Donald Trump la kutaka Urusi irudishwe katika kundi la mataifa saba yenye uwezo mkubwa wa kiuchumi duniani (G7).

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas, katika mahojiano yaliyochapishwa kwenye gazeti la Rheinische Post alisema haoni uwezekano wa Urusi kurudishwa katika G7 hivi karibuni, kufuatia pendekezo la Rais Trump.

"Sababu ya Urusi kutolewa katika kundi la G7 ni uingiliaji wake katika eneo la mashariki mwa Ukraine, na kuiteka rasi ya Crimea. Kama bado hakujapatikana suluhu huko, sioni nafasi ya kuiruhusu tena Urusi ndani ya G7," alisema Maas.

Urusi iliondolewa kutoka kundi la G7 mwaka 2014 baada za Moscow kuiteka rasi ya Crimea kutoka kwa Ukraine.

Rais Trump alipendekeza upanuzi wa nchi za G7 na tayari amesema anapanga kuzialika Australia, India, Urusi na Korea Kusini kwa mkutano unaofuata wa G7 ambao anapanga kuwa mwenyeji Septemba.

Mkutano huo uliahirishwa awali kutokana na janga la virusi vya corona. G7 lilikuja pamoja mwaka 1975 kama mataifa saba muhimu yaliyoendelea zaidi kiviwanda wakati huo.

Nchi wanachama wa G7 ni Uingereza, Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan na Marekani. Mwaka 1998 Urusi iliongezwa kwenye kundi hilo na kuwa G8 lakini baadaye iliondolewa.

Maas alisema uhusiano na Urusi kwa wakati huu ni mgumu katika kila sehemu. Juu ya hayo, ameikosoa Urusi kwa kuzuia kupelekwa kwa misaada ya kibinadamu kwa kiasi ya watu milioni 1.5 nchini Syria.

Waziri huyo wa Mambo ya Nje wa Ujerumani ameitolea wito Urusi kuongeza juhudi za kumaliza mzozo mashariki mwa Ukraine, Syria na Libya. **DW**

## International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

**DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014**
**MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES As at 30th June 2020**

| PRODUCT TYPE | TZS | USD | GBP | EUR |
|---|---|---|---|---|
| **SERVICES** | | | | |
| Monthly Statement Current Accounts | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement Savings Accounts | Free | Free | Free | Free |
| E-statement | Free | Free | Free | Free |
| Interim statement - per page | 1,000 | 1 | 1 | 1 |
| **MINIMUM ACCOUNT OPENING** | | | | |
| Savings Account-Salaried | Free | Free | Free | Free |
| Savings Account-Normal | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| Current account-Normal | 50,000 | 100 | 100 | 100 |
| Current account -Premium | 1,000,000 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| **CASH WITHDRAWALS OVER THE COUNTER** | | | | |
| Savings account - A | | | | |
| I. Above 500,000 | Free | NA | NA | NA |
| II. Less than 500,000 | 1,000 | NA | NA | NA |
| Savings account - B | | | | |
| I. Up to USD/GBP 10,000 | NA | 5 | 5 | 5 |
| II. Above USD/GBP 10,000 | NA | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| | | | | |
| Current account | | | | |
| I. Up to 5,000,000 | Free | NA | NA | NA |
| II. Above 5,000,000 | 2,000 | NA | NA | NA |
| Current account | | | | |
| I. Up to USD/GBP 10,000 | NA | 5 | 5 | 5 |
| II. Above USD/GBP 10,000 | NA | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| Third Part withdraw per leaf | 30,000 | 30 | 30 | 30 |
| **CASH HANDLING FEE** | | | | |
| Deposits on Small Denominations Less than $50 | 3% | 3% | 3% | 3% |
| | | | | |
| **ATM WITHDRAWALS** | | | | |
| On Us | 600 | NA | NA | NA |
| On Others | NA | NA | NA | NA |
| **OTHER ATM TRANSACTIONS** | | | | |
| Issue of ATM Card(New) | 6,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card (faulty) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card (worn out) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card(Lost) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| **TRANSFERS** | | | | |
| Internal transfers | Free | Free | Free | Free |
| Interbranch Transfer | Free | Free | Free | Free |
| **STANDING ORDERS** | | | | |
| Standing orders (within bank) | 1,500 | 0.50 | 0.50 | 0.50 |
| Standing orders (to other banks Local Currency ) | 11,800 | NA | NA | NA |
| Standing orders (to other banks ) below usd 10,000 | NA | 3 | 3 | 3 |
| Standing orders (to other banks ) above usd 10,000 | NA | 10 | 10 | 10 |
| Unpaid standing orders | 40,000 | 20 | 20 | 20 |
| **CHEQUES** | | | | |
| Cheque book issuance | | | | |
| I. Personal chq book with 25 leaves | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| II.Corporate chq book with 50 leaves | 50,000 | 20 | 20 | 20 |
| III.Corporate chq book with 100 leaves | 70,000 | 35 | 35 | 35 |
| Counter cheque charges per leaf | 20,000 | 20 | 20 | 20 |
| Stop Payment orders -per instructions/ Cheque series | 40,000 | 20 | N/A | N/A |
| **Outward Cheque Unpaid (Chq returned by Us)** | | | | |
| I. Refer to Drawer | 50,000 | 50 | N/A | N/A |
| II. Effect not Cleared | 30,000 | 30 | N/A | N/A |
| III. Any Technical reason (Like endorsement) | 10,000 | 5 | N/A | N/A |
| **Inward Cheque Unpaid (Chq returned by other bank)** | 10,000 | 5 | N/A | N/A |
| Inward Cheques processing per leaf | 500 | 1 | N/A | N/A |
| | | | | |
| Bankers Cheque (account holders) | 15,000 | 10 | N/A | N/A |
| Re- Purchase of Bankers cheque on customers request | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Uncollected Cheque book (after one Month) | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| **OTHER SERVICES** | | | | |
| Current Account Closure on customer's request | 30,000 | 15 | 15 | 15 |
| Savings Account Closure on customer's request | 20,000 | 5 | 5 | 5 |
| Cheque Force clearance (with one day float) | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Chq Force clearance (with more than one day float) | 40,000 | 20 | 20 | 20 |
| Dormant Charges for Savings account | Free | Free | Free | free |
| Dormant Charges for current account | 25,000 | 15 | 15 | 15 |
| Dormant account Activations | Free | Free | Free | free |
| Account Maintanance Charge - Savings | 1,000 | 2.50 | 2.50 | 2.50 |
| Account Maintanance Charge - Current | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| Certificate of balance | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Letter of introduction | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Salary handling | Free | Free | Free | free |
| School fees deposits | Free | Free | Free | Free |
| Un arranged Temporary Overdrafts (TODs) | 24% | 10% | 10% | 10% |
| Corporate Premier Account Maintanance Charge | 20,000 | 20 | N/A | N/A |
| Individual Premier Account Maintanance Charge | 20,000 | 20 | N/A | N/A |
| Lost Cheque charges | 20,000 | 18 | 18 | 18 |
| EFT charges: | | | | |
| On Us | 300 | Free | N/A | N/A |
| On Others | 11,800 | NA | N/A | N/A |
| **TRADE FINANCE** | | | | |
| **Remittance** | | | | |
| Demand draft | NA | NA | NA | NA |
| Outward Local transfers ( TISS) | 11,800 | 11.80 | NA | NA |
| Outward Foregin transfers -Up to USD50,000 | NA | 50 | 50 | 50 |
| Outward Foregin transfers - above USD50,000 | NA | 75 | 75 | 75 |
| Inward Local transfer (TISS) | Free | Free | Free | Free |
| Inward Foreign transfer | NA | 15 | 15 | 15 |
| **Bonds & Guarantees** | | | | |
| Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Extentions | 1.42% Per Quarter | | | |
| Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| Cancellations of guarantees if not Returned | 20,000 | | | |
| **Advance Payment Guarantees** | | | | |
| Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance swift charges | Usd 50 | | | |
| **Export Collections (EC)-Outward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance Commission-per tracer | Usd 50 | | | |
| Courier Charges | Usd 100 | | | |
| **LOAN & ADVANCES** | | | | |
| Loan Processing Fees | 1.82% | | | |
| Early Loan Repayment Charges | 1% | | | |
| | | | | |
| **BASIC LENDING RATE** | 24% | 10% | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

| | | |
|---|---|---|
| Villy Vellayappan | Chief Executive Officer | 22.07.2020 |
| Christome Tembo | Head of Operation | 22.07.2020 |
| John Mwakasonda | Head of Internal Audit | 22.07.2020 |

## HABARI MICHEZO



# DYBALA AKARIBIA KUSAINI MKATABA MPYA

**TURIN,** Italia

JUVENTUS "wamefikia pazuri" kuhusu mazungumzo ya mkataba mpya na Paulo Dybala, kwa mujibu wa mkurugenzi wa soka wa klabu hiyo, Fabio Paratici.

Dybala mwenye umri wa miaka 26, mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022, lakini amekuwa akihusishwa kupewa mkataba mpya bada ya kuwa na msimu wa kufurahisha hapo Turin.

Paratici amethibitisha mazungumzo na Dybala yalikuwa yanendelea na sasa mchezaji huyo anajiandaa kubakia hapo Juve.

"Mara kwa mara tunazungumza na wawakilishi wake na tunasonga mbele, licha ya magumu yaliyotokea, lakini mambo yanakwenda vizuri," alisema akiiambia Sky Sport.

"Hata wakati huu, tumekuwa tukizungumza mara kwa mara na mazungumzo yanaendelea vizuri."

Juve ilitwaa taji la tisa la Serie A Jumapili shukrani kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sampdoria.

# Arteta ataka walinzi watatu Arsenal

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema Arsenal itahitaji kuimarisha safu ya ulinzi ya kati baada ya kubainisha kwamba, Shkodran Mustafi atakosa mwanzo wa msimu huu kutokana na majeruhi.

Mustafi aliumia kwenye mchezo wa nusu fainali ya kombe la FA wakati wakishinda dhidi ya Manchester City na awali alitarajiwa kukaa nje ya dimba kwa kipindi cha wiki kadhaa.

Arteta amethibitisha kwamba majeruhi yake yatamweka nje ya dimba kwa muda mrefu baada ya mchezo wa ushindi wa Jumapili dhidi ya Watford, hata hivyo, raia huyo wa Ujerumani atakuwa nje ya wiki kwa wiki kadhaa.

Alipoulizwa kama Mustafi ataukosa mwanzoni mwa msimu ujao, ambao unatarajiwa kuanza Septemba 12, Arteta aliwaambia waandishi wa habari: "Ndio, tutamkosa.

"Inaumiza. Aliumia nyama za paja na hilo litamuweka nje ya dimba kwa wiki kadhaa na tutamkosa."

Arsenal pia imekuwa bila ya walinzi wenzake wa kati, Calum Chambers na Pablo Mari kutokana na majeruhi ya muda mrefu, huku wachezaji wote wakiwania kuwa fiti kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Na licha ya ujio wa William Saliba kutoka Saint-Etienne, Arteta anaelewa kwamba anahitaji kuleta mchezaji mwingine wakati wa dirisha la usajili la majira haya ya joto.

"Tayari nimeshatajiwa walinzi wa kati watatu ambao hawapo na sijakuwa nao kwa muda mrefu kwa msimu huu," alisema na kuongeza: "Tutaliangalia hilo kwa umakini mkubwa."





# *Mourinho kuijenga upya Tottenham*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho anaangalia uwezekano wa kuimarisha kikosi cha Tottenham Hotspur kwa ajili ya msimu ujao baada ya kumaliza msimu kwa kufuzu kucheza Ligi ya Europa.

Sare ya 1-1 dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja la London, Crystal Palace iliwatosha Spurs kumaliza juu ya Wolves, waliofungwa 2-0 na Chelsea katika siku ya mwisho ya msimu huo na kumaliza wakiwa nafasi ya sita.

Baada ya kushinda mechi nne na kutoa sare mbili katika mechi sita za mwisho, Mourinho anahisi kikosi chake kina uwezo wa kumaliza kwenye nne bora msimu ujao, lakini watahitaji sura mpya kutokana na kukabiliwa na majeruhi.

"Wakati wachezaji wote walikuwapo tumeonyesha katika kipindi hiki cha mwisho wapi tunapotakiwa kuwapo," alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Baada ya "lockdown" tulimaliza kwenye nafasi ya tatu au nne kwenye msimamo. Hiyo ndio sehemu tuliyotakiwa kuwepo. Nataka kuwa na timu yangu, wachezaji wangu wakiwa uwanjani badala ya kuwa kwenye vyumba vya hospitali.

"Tunataka kubakiwa na wachezaji wetu wazuri baada ya kuonyesha kuimarika kwenye kikosi. Tutakwenda kununua wachezaji 10? Hapana, tunakwenda kulipa pauni milioni 100 kwa mchezaji? Hapana.

"Lakini ngoja tuone. Soko ni la ajabu sana. Sijui kama tutaanza kipindi cha maandalizi ya msimu na mchezaji mpya au kitu ambacho kitatuwezesha kwenda msimu wote.

"Tunakwenda kutengeneza muundo wa timu kwa sababu, hatuna mpango wa kuuza wachezaji wetu bora."

HABARI MICHEZO

# Sancho kurudi mazoezini Dortmund

**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho anatarajia kurudi kwenye mazoezi na Borussia Dortmund wiki hii, huku kukiwa na ripoti kwamba kuna uwezekano wa kuhamia Manchester United.

Nyota huyo wa timu ya taifa ya England amekuwa akihusishwa na mashetani wekundu hao licha ya Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa United, Ed Woodward akiwa ameonya kwamba ni vigumu kuingia kwenye usajili wa kutumia fedha nyingi, hasa baada ya hadhari ya mlipuko wa virusi vya corona.

United ilimaliza ligi ikiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Leicester City.

Huku sasa klabu hiyo itapata ahuweni ya fedha kwa kufuzu kucheza mashindano hayo ya Ulaya, kuna uwezekano mkubwa wa usajili kufanyika pale Old Trafford kwa ajili ya kuimarisha kikosi, huku wakiwania kumshawishi Sancho ndani ya wiki zinazokuja.

Ingawa kwa sasa, Mkurugenzi wa Michezo wa Dortmund, Michael Zorc hatarajii kupokea ofa kwa ajili ya winga huyo mwenye umri wa miaka 20.

Dortmund wanadai kwamba wanataka kiasi cha euro milioni 100 kwa ajili ya Sancho, ada ambayo United wanataka ipunguzwe.

Sancho alimaliza Ligi Kuu ya Ujerumani kwa kiwango cha kuvutia akiwa amefunga mabao 17 na pasi za mwisho 16 kwenye mechi 32 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Dortmund ilimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo, ikipitwa pointi 13 na vinara Bayern.





# LAMPARD KUAMUA HATIMA YA KEPA

**LONDON,** England

FRANK Lampard atasubiri hadi mwisho kabisa wa msimu huu kufanya tathmini ya kikosi chake baada ya kumuacha golikipa, Kepa Arrizabalaga kwenye mechi ya mwisho wa msimu huu, Jumapili.

Kepa mwenye umri wa miaka 25, amekalia kuti kavu baada ya kushuka kiwango msimu huu na nafasi yake ilichukuwa na Willy Caballero kwenye kikosi cha kwanza, wakati Chelsea wakiifunga Wolves 2-0 kwenye mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu Jumapili, na kumaliza kwenye nne bora.

Chelsea itacheza na Arsenal kwenye fainali ya kombe la FA Jumamosi na baadaye itakutana na Bayern Munich kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16, wakiwa wamepoteza 3-0 katika mchezo wa kwanza.

Lampard amesema bado hajafanya maamuzi juu ya golikipa wake, huku klabu ikihusishwa kumuwania kipa wa Atletico Madrid, Jan Oblak.

"Ni wazi kwamba, tumeshinda kuzuia mabao mengi na sio kwa sababu ya kipa pekee, ni kitu ambacho tunatakiwa kukifanyia kazi kama timu, kuangalia namna gani tunajifua na jinsi ya kuwatengeneza mafowadi wetu," alisema kocha huyo wa Chelsea akiwaambia waandishi wa habari.

"Sitaki kumtaja Kepa. Suala la Kepa yalikuwa maamuzi ya kuchagua, pengine kwa kiwango cha hivi karibuni, muda mgumu kwake.

Kepa alikuwa golikipa ghali zaidi duniani wakati alipowasili Chelsea kutoka Athletic Bilbao kwa ada ya pauni milioni 71.6 mwaka 2018.

# *Ushindi wa Juventus ulikuwa mgumu-Sarri*

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri ameutaja ushindi mara tisa wa Juventus wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A kama "mafanikio yasiyotarajiwa."

Mabao kutoka kwa Cristiano Ronaldo, ambaye alikosa penalti, na lile la Federico Bernardeschi yaliisaidia Juve kupata ushindi wa 2-0 dhidi ya Sampdoria Jumapili na kulibeba taji hilo.

Utawala wa Sarri na Juve ulikuwa wa aina yake, akiwasifia wachezaji wake kwa kushinda Serie A baada ya ligi kusimama kwa zaidi ya miezi mitatu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Ulikuwa mmoja wa msimu mgumu zaidi, kwa sababu ya kila kitu kilichotokea," kocha huyo mkuu wa Juventus aliwaambia waandishi wa habari.

"Kama unafikiri tulianza maandalizi ya msimu mpya Julai 6, na tumeshinda taji Julai 26 ni mwaka mmoja, hiyo ni ngumu. Hakuna mtu anayeweza kuniambia kwamba ni siku 50, 60.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Napoli, Sarri mwenye umri wa miaka 61 amekuwa kocha mzee zaidi kushinda taji la Serie A.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AMSIFIA FERNANDES MAN U

## ●●● Asema wanatakiwa kukubali kwamba, amekuja na kutoa mchango mkubwa kwa...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amepaza sauti kusifia "mchango mkubwa" wa Bruno Fernandes baada ya kiwango chake kuwasaidia mashetani wekundu hao kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

**Pia Man United imefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.**

Fernandes alifunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 71 na Jesse Lingard aliyetokea benchi akafunga la pili wakati United ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Leicester, Jumapili.

Baada ya Anthony Martial kufanyiwa faulo na Jonny Evans ndani ya eneo la hatari, Fernandes alichukua mpira na kupiga penalti wakati zikiwa zimesalia dakika 19 mpira kumalizika pale kwenye dimba la King Power, ambapo Lingard akamaliza kufunga.

Fernandes ameimarisha United tangu alipotua hapo Januari akitokea Sporting CP ya Ureno - na kiungo huyo nyota amefunga mabao nane ya Ligi Kuu na pasi za mwisho saba.

Kiwango chake hicho ndio kwa kiasi kikubwa kilichoisaidia timu hiyo ya Solskjaer kumaliza kwenye nne bora ya msimmo wa ligi wakitoka nafasi ya tano, wakipitwa pointi 14 na tofauti ya mabao 20 na Leicester mapema Januari Mosi baada ya kichapo kutoka kwa Arsenal.

"Tunatakiwa kukubali kwamba, amekuja na kutoa mchango mkubwa mno kwa timu. Mchango wake umeisaidia sana timu," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Amekuwa akifunga mabao ya kuvutia, akitengeneza mabao, lakini pia, akichangia kasi ya timu yote.

"Pengine leo unaweza kumuona Bruno amechoka, na hilo ni kawaida kwa sababu amecheza mno.

"Unaweza kuona hamasa yake. Mchango wake umesaidia sana timu na sio mzungumzaji uwanjani zaidi ya vitendo. Ameitoa timu kutoka mbali na kwa hakika kabisa amechangia sisi kumaliza kwenye nne bora."

## ZISIKUPITE

### AJIFUNGA SOUTHAMPTON

KIUNGO wa kati wa Southampton, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 25, amekubali dili jipya ambalo litamfanya kusalia na klabu hiyo hadi mwaka 2025. ***(Telegraph)***

### BARNES AWINDWA LEICESTER

WINGA wa Leicester City na timu ya taifa ya England kwa wachezaji wa chini ya miaka 21, Harvey Barnes, anawindwa kusajiliwa na Liverpool. ***(Mirror)***

### LIVER YAJITOSA KWA OZAN

LIVERPOOL inamfuatilia beki wa kati wa Schalke na Utueuki, Ozan Kabak, ambaye awali alikuwa akiwavutia Manchester City, Juventus na Borussia Dortmund. ***(Mail)***

### DORTMUND YAMTAKA IKONE

KLABU ya Borussia Dortmund imeanza mazungumzo kwa ajili ya kiungo mshambuliaji wa Lille, Jonathan Ikone mwenye umri wa miaka 22, wakitaka kumfanya kuwa mbadala wa winga Jadon Sancho mwenye miaka 20, ambaye amekuwa akihusishwa na taarifa za kuhamia Manchester United. ***(Times)***

### ARTETA KUTAFUTA BEKI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amedokeza kuwa anaweza kuingia kwenye soko la usajili kutokana na jeraha la mchezaji wa nafasi ya ulinzi, Mjerumani Shkodran Mustafi mwenye umri wa miaka 28, hali ambayo imemfanya kuwa na upungufu wa wachezaji wa safu ya ulinzi. ***(Evening Standard)***

### LEEDS YAMWANIA DAVID

LEEDS United wanajaribu kumsajili kiungo mshambuliaji wa Gent, Jonathan David mwenye miaka 20, huku wakikabiliwa na ushindani kutoka Lille, kwa mujibu wa Mwenyekiti wa klabu hiyo ya Ubelgiji, Ivan de Witte. ***(De Zondag, via Express)***

### CAVANI MDOMONI MWA LEEDS

MSHAMBULIAJI wa Uruguay Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 33, amekuwa akiwindwa na Leeds baada ya kuondoka Paris St-Germain, lakini amekubali kuelekea katika klabu ya Ureno, Benfica ***(Todo Fichajes)***

### SEAN KUMRITHI HODGSON

KLABU ya Crystal Palace inawania kumchukua kocha wa Burnley, Sean Dyche ili awe mrithi wa Roy Hodgson. ***(Sunday Mirror)***

### MAN U KUMHAMISHA OBLAK

KLABU ya Manchester United inapanga kufanya uhamisho wa golikipa wa Atletico Madrid na Slovenia, Jan Oblak mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

### INTER KUMBADILISHA PERISIC

KLABU ya Inter Milan inaweza kutoa ofa ya kiungo wa Croatia, Ivan Perisic mwenye umri wa miaka 31 kwa Manchester United ili kumsajili moja kwa moja, Alexis Sanchez anayecheza kwa mkopo. ***(Football Italia)***

HABARI MICHEZO

## Katwila cheko tupu Mtibwa kubaki EPL

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema amefurahi kuona timu yake inaendelea kubaki katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nina shukuru timu yangu haijashuka daraja bado tutaendelea kuwapo Ligi Kuu kikubwa japo kuwa msimu ulikuwa na ushindani mkubwa," alisema Katwila.

Katwila alisema baada ya kumaliza msimu huu ataanza moja kwa moja mikakati ya usajili kwa ajili ya kukipa nguvu kikosi hicho ili kiwe na nguvu msimu ujao.

"Msimu huu tunashukuru tumemaliza salama nitaanza mapema maandalizi kwa ajili ya msimu ujao ili nirudi kivingine msimu huo," alisema.

Katika hatua nyingine alisema makosa ambayo yalijitokeza katika msimu uliopita atayafanyia kazi ili yasijitokeze kwa mara nyingine msimu ujao.

## Dodoma yachimba mkwara Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC, umepania kuhakikisha timu yao inabakia kwenye Ligi Kuu Tanzania, kwani imepanda kwa ajili ya kushindana na si kuwa msindikizaji.

Akizungumza na gazeti hili Katibu Mkuu wa timu hiyo, Johnson Fourtnatus alisema wameweka mikakati kuhakikisha wanaleta ushindani kwenye ligi hiyo msimu ujao. Alisema watahakikisha kubaki na kucheza ligi kila msimu baada ya sasa kutaka kufanya usajili wa kuboresha kikosi chao.

"Sisi tumekuja kuleta ushindani na changamoto kwa timu zingine hivyo malengo yetu ni makubwa, hatuwezi kuingia katika mfano wa timu iliyopanda na kucheza msimu mmoja na kushuka," alisema katibu huyo.

Alisema tayari wamepokea ripoti ya benchi la ufundi na kujadili wachezaji waliopendekezwa na kuangalia ni sehemu gani wanatakiwa kuboresha.

Katibu huyo alisema hawatarajii usajili wao kujaza wachezaji waliotemwa na timu za Ligi Kuu na zaidi wanaangalia vijana wanaochipukia watawasaidia kuleta ushindani.

Dodoma Jiji FC ni mabingwa wa ligi daraja la kwanza baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Gwambina FC mechi ya fainali iliyopigwa Jumamosi iliyopita uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

# SENZO: JUHUDI ZIMEIPA SIMBA SC UBINGWA

**Na Somoe Ng'itu,** MOSHI

BAADA ya timu yao kumaliza msimu wa mwaka 2019/20 kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania, uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba umesema kikosi chao kilistahili kutetea ubingwa wa ligi hiyo kutokana na kiwango kizuri walichokionyesha kwenye michezo mbalimbali msimu huu.

**Simba imemaliza msimu huu ikiwa na pointi 88 huku nafasi ya pili ikichukuliwa na Yanga iliyojikusanyia pointi 72 na Azam FC imefuata ikiwa na pointi 70.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha, alisema ulikuwa msimu mgumu lakini kikosi chao kilipambana kuhakikisha wanaibuka na ushindi na hatimaye wanatimiza malengo waliyojiwekea wakati wanaanza msimu.

Mbatha alisema wachezaji walijaribu kuonyesha juhudi na uzoefu pale walipopoteza mchezo na kurejea uwanjani wakiwa na kasi mpya kwenye mechi iliyofuata.

"Msimu ulikuwa mgumu sana, ulikuwa na ushindani na changamoto mbalimbali, haikuwa kazi rahisi kufikia hapa, napenda kuwapongeza wachezaji na wafanyakazi wote wa Simba, bado tunahitaji kwenda kumalizia kazi katika mechi ya fainali ya Kombe la FA," alisema kiongozi huyo.

Alieleza kikosi hicho kimejipanga kuhakikisha wanamaliza msimu huu kwa kutwaa taji la tatu na wamejiandaa kuonyesha kwamba wanastahili kupata ushindi.

"Simba inaimarika kadri siku zilivyokuwa zinakwenda, kuna wakati walicheza vibaya, lakini Sven alifanikiwa kubadilisha mchezo na kurejea katika ubora wao, wamefanya kazi nzuri sana, tumestahili kuwa hapa tulipo," Mbatha alisema.

Alisema kikosi chao kilitarajiwa kurejea jijini Dar es Salaam jana asubuhi na baadaye kuelekea Mbeya kuweka kambi ya muda mfupi ili kuifuata Namungo katika mchezo wa fainali ya Kombe la FA itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga mjini Rukwa.

"Tutawakosa wachezaji wawili, akiwamo Tairon, ambaye ni majeruhi, hata leo (juzi) umeona kocha amechezesha timu iliyojiandaa na fainali ingawa uwanja (Chuo cha Ushirika) haukuwa rafiki, tunaenda Sumbawanga kukamilisha kazi," Mbatha aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema bao la mapema lililofungwa na nahodha wa Simba, John Bocco liliwatoa mchezoni na kukifanya kikosi chake kipoteze mechi hiyo.

"Tulizidiwa, tulicheza katika kiwango cha chini, Simba walituzidi kwenye idara ya kiungo na ulinzi, walifanikiwa kutubana," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa atazungumza na mabosi wake kuhakikisha wanawabakisha wachezaji wote wanaowahitaji ili kukiandaa kikosi imara cha msimu ujao.

Msimu wa 2019/20 umemalizika huku tukishuhudia Alliance FC, Ndanda, Lipuli na Singida United zikiteremka moja kwa moja wakati Mbao na Mbeya City hatima yao itajulikana baada ya mechi za mtoano.



Wapiga vyombo wa bendi ya Waluguru Original ya mjini Morogoro akiwamo mpiga besi mzee Magati (kushoto) wakifanya vitu vyao kwenye onyesho la bendi hiyo mjini humo hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Uwiano wa magoli ulivyoamua timu za kushuka*

**Na Adam Fungamwango**

UMUHIMU wa kuwa na magoli mechi ya kufunga, lakini kutoruhusu magoli mengi kwenye Ligi Kuu ulionekana kwenye mechi za mwisho wa Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kanuni hiyo kuamua timu za kushuka, zilizoenda kucheza mechi za mchujo na zilizobaki Ligi Kuu.

Ilikuwa ni patashika nguo kuchanika kwenye mechi za mwisho, kila timu ikihitaji kushinda, huku zikiombeana mabaya, lakini hatimaye timu za Ndanda FC, Lipuli na Alliance FC zilijikuta zikiteremka daraja moja kwa moja na kungana na Singida iliyokuwa imeshashuka siku nyingi, lakini Mbao FC, Mbeya City zikiponyeka kwenye tundu la sindano na kwenda kucheza mechi za mchujo, huku Mtibwa Sugar ikibahatika kubaki salama salimini.

Jumla ya timu nne ambazo ni Alliance FC, Mbao FC, Mbeya City na Mtibwa Sugar zote zilimaliza mechi zao za ligi zikiwa na pointi 45 kila moja.

Kilichoifanya Alliance FC ishuke daraja, Mbeya City na Mbao FC, kwenda kwenye mechi za mchujo na Mtibwa Sugar kubaki Ligi Kuu ni uwiano tu wa magoli ya kufunga na kufungwa.

Timu ambazo zimeshuka kutokana na kuwa na pointi chache ni Singida United iliyoshuka na pointi 18, Ndanda FC pointi 41 na Lipuli ikimaliza na pointi 44.

Kilichoishusha Alliance, pamoja na kuwa na pointi 45 kama wenzake ni kuwa na hasi 12. Timu hiyo imefunga magoli 36 na kufungwa magoli 48, hivyo wanadaiwa magoli 12 na kukaa kwenye nafasi ya 17.

Mbao FC imekwenda kwenye mechi ya mchujo kucheza na Geita Gold kwa sababu ina hasi 10, imefunga magoli 33 na kufungwa 43, kwa maana hiyo inadaiwa magoli 10 na kushika nafasi ya 16.

Mbeya City, pointi sawa na wenzake, lakini inakamata nafasi ya 15 na kwenda kwenye mchujo kwa sababu ina magoli 33, lakini imefungwa magoli 42, kwa maana hiyo inadaiwa au ina hasi ya magoli tisa.

Mtibwa Sugar imeponea chupuchupu kutokana na tu na kuwa na hasi nne, ikiwa na pointi hizo hizo 45, lakini imefunga magoli 30 na kufungwa 34, hivyo uwiano mdogo wa magoli ya kufungwa dhidi ya wenzake ndiyo ulioikoa timu hiyo, iliyomaliza ligi kwenye nafasi ya 14.

Michezo

Jumanne Julai 28, 2020

Nipashe



Solskjaer amsifia Fernandes UKURASA 22

# FIFA kumshukia Eymael

●●● Yanga yamtimua kwa kutoa kauli zinazokiuka...

**Isaac Kijoti,** IRINGA **na Somoe Ng'itu,** MOSHI

LICHA ya sifa kubwa aliyoipata juzi kwa kuishusha Lipuli FC daraja ikiwa katika Uwanja wake wa Samora mjini hapa baada ya kuichapa bao 1-0, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amemwaga mboga na klabu yake hiyo kuamua kumwaga ugali kwa kumfuta kazi.

**Kabla ya mechi ya juzi ambayo Yanga ilikuwa ikihitaji ushindi ili kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara huku Lipuli ikihitaji kushinda ili kuepuka kushuka daraja, Eymael alinukuliwa katika mitandao ya kijamii na vyombo vya habari akitoa kauli za vitendo vya kibaguzi kwa mashabiki wa klabu hiyo.**

Baadhi ya kauli alizozitoa Eymael ni pamoja na kueleza mashabiki kuwa hawana elimu huku akiongeza, "watu kwenye nchi hii ni wapumbavu, mashabiki hawajui mpira kazi yao ni kupiga kelele kama nyani na huku wakibweka kama mbwa, viongozi wa klabu ni sifuri na Shirikisho la Soka Tanzania lipo kwa ajili ya Simba tu.

"Soka linachezwa katika viwanja vibovu, viwanja kama hivi havifai, niliwaambia Yanga waache nimalize ligi niondoke hata mke wangu hana furaha, niacheni niondoke," amenukuliwa kocha huyo ambaye juzi alishangiliwa vilivyo na mashabiki wa Yanga baada ya kuiwezesha kumaliza nafasi ya pili, shukrani kwa David Molinga aliyeizamisha Lipuli.

Hata, hivyo Yanga jana ilichukua hatua mara moja baada ya kutoa taarifa kwa vyombo vya habari ikieleza kutokana na kauli hizo za kibaguzi wameamua kumfuta kazi Eymael kuanzia leo (Julai 27, 2020) na kuhakikisha anaondoka nchini haraka iwezekanavyo.

"Uongozi wa Klabu ya Yanga umesikitishwa na kauli zisizo za kiungwana na za kibaguzi zilizotolewa na kocha wake, Luc Eymael na kusambaa katika mitandao ya kijamii," ilieleza taarifa hiyo.

Mbali na hatua hiyo, uongozi wa Yanga umewaomba radhi viongozi wa nchi, TFF, viongozi wa Klabu ya Simba, wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga, pamoja na wananchi kwa ujumla kutokana na kauli za kuudhi na kudhalilisha zilizotolewa na kocha huyo.

"Klabu ya Yanga inathamini na kuamini katika misingi ya nidhamu na utu, na inapingana na aina yoyote ya ubaguzi," ilieleza zaidi taarifa hiyo iliyotolewa na kusainiwa na Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Wakili Simon Patrick.

Katika hatua nyingine TFF, nayo haikutaka kumung'unya kauli katika suala hilo baada ya jana kutoa taarifa kwa vyombo vya habari ikieleza litamchukulia hatua za kinidhamu Eymael kwa kumfikisha katika vyombo husika kutokana na kutoa matamshi ya kibaguzi kwa mashabiki wa timu hiyo.

TFF imeeleza itafikisha taarifa hizo kwa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kuhusu kauli hizo ili nalo limchukulie hatua kwa kuwa bado anaweza kufanya vitendo hivyo katika nchi nyingine.

"Mwaka jana FIFA ilifanya marekebisho ya kanuni zake kinidhamu na kuongeza adhabu kwa wanaofanya vitendo vya kibaguzi kwa vile ni ukiukwaji mkubwa wa haki za msingi za binadamu," ilieleza taarifa hiyo iliyotolewa na Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo.

**MEXIME AITWA**

Wakati huo huo, taarifa zaidi zinasema kwamba uongozi wa Yanga umemuita kocha wa Kagera Sugar, Mecky Mexime ili kuchukua mikoba ya kukinoa kikosi hicho.

Awali iliripotiwa kwamba, Yanga walimpa mkataba Mexime na alikuwa anatembea nao na kwamba yale yote aliyokuwa akiyataka, walikuwa tayari kumpatia.



Luc Eymael

# MO atuma maombi kwa JPM

**Na Sanula Athanas**

MFANYABIASHARA maarufu, Mohamed Dewji 'MO', ameanzisha maombi kwa Rais John Magufuli kubadili jina la Uwanja wa Taifa kuwa Uwanja wa Benjamin William Mkapa.

MO, miongoni mwa mabilionea vijana barani Afrika na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, amesema maombi yake hayo yamezingatia historia ya ujenzi wa uwanja huo mkubwa zaidi nchini.

Akirejea historia hiyo, MO alisema jana kuwa ujenzi wa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ulianzishwa na Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia Ijumaa.

Uwanja huo uliojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 56 kwa ushirikiano wa Tanzania na Serikali ya Watu wa China, una uwezo wa kuketisha mashabiki 57,558 na ni miongoni mwa viwanja bora barani Afrika kwa sasa.

"Uwanja huo kwa namna mmoja au nyingine umesaidia kuendeleza mpira wa miguu na michezo mingine nchini. Uzuri na ukubwa wa soka letu umedhihirishwa kwa sababu ya uwanja wetu huo ambao unashika nafasi ya 11 kwa ukubwa Afrika," MO alisema.

"Uwanja huo wa kisasa umeongeza uzalendo mkubwa kwa kuwezesha maelfu ya mashabiki kuwa sehemu ya michezo yote mikubwa, pia umeongezea mapato kwa klabu zote na kutuletea heshima kubwa nchini na mifano ipo dhahiri.

"Kutokana na uzuri wa uwanja huo, klabu zote za nje ambao huja kucheza katika uwanja huo zimekuwa zikitoa sifa mbalimbali. Timu za mataifa makubwa kama Brazil zimecheza kwenye uwanja huo na kumwaga sifa mbalimbali.

Alisema itakuwa ni heshima kubwa kama uwanja huo utaitwa kwa jina la Benjamin William Mkapa, akimwomba Rais Magufuli aridhie kubadili jina la uwanja huo kwa heshima ya Hayati Mkapa, ili kuendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa na hasa kwa vizazi vijavyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >